USAWIRI WA UJINSIA KATIKA FILAMU: UCHUNGUZI WA MATUMZI YA LUGHA KATIKA FILAMU ZA STEVEN KANUMBA

AHMAD ABDALLA SUWED

IMEWASILILISHWA KAMA SHARTI PEKEE LA KUHITIMU SHAHADA YA UZAMILI (M.A) YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2013

ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo: **"Usawiri wa Ujinsia Katika Filamu: Uchunguzi wa Matumzi ya Lugha Katika Filamu za Steven Kanumba",** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

____

Prof. Emmanuel Mbogo

(**Msimamizi**)

Tarehe: __________________

HAKI MILIKI

Haki ya kunakili tasinifu hii inalindwa na Mkataba wa Berne, Sheria ya Haki ya Kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali za kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya Tasnifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea, au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

IKIRARI

Mimi **Ahmad Abdalla Suwed**, nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu ya halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Digrii yoyote.

Saini _______________________

Tarehe _______________________

TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu kwa mapenzi yao kwangu na kunisomesha hadi leo nimefikia hatua hii kitaaluma.

SHUKRANI

Kwanza kabisa kabla napenda kutoa shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu Allah Subhanahu Wataalah kwa kunijaalia afya njema kipindi chote cha masomo yangu, kunipa nguvu, uwezo, akili, busara na maarifa katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Nasema kwa unyenyekevu mkuu, Alhamdulillah Rabbilaalamina.

Pili, shukurani za pekee ni kwa wazazi wangu kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha. Kwa uvumilivu wao kuwa mbali nami hasa katika kipindi chote nilichoishi Tanzania kwa ajili ya masomo yangu ya uzamili. Nawaombea maisha marefu yenye afya na baraka tele!

Tatu, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Msimamizi wangu Prof. Emmanuel Mbogo kwa kunilea kitaaluma na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili. Kunifunza na kunipa miongozo juu ya filamu. Namuombea afya njema na maisha marefu ili walio azidi kuwa hazina ya taaluma kwa wenye kiu ya kuitafuta.

Nne, napenda kuwashukuru wahojiwa wangu wote walioshiriki katika utafiti huu kwa ukarimu na ushirikiano walionipa kipindi chote nilichokuwa uwandani. Nitakuwa mchahe wa fadhira nisipotoa shukrani zangu kwa watanzania wote walionifunza Kiswahili nikaweza kuishi bila shida Tanzania. Namshukuru Bi. Hadija Jilala kwa kunifunza lugha ya Kiswahili na kunipa changamoto za kitaaluma juu ya filamu ya Kanumba na hasa mswada wake wa Kanumba na Fasihi ya Kiswahili ambao ulinipa chachu ya kutafiti eneo hili kwa kutumia filamu za Kanumba.

Nitakuwa mchache wa fadhira nisipotoa shukurani kwa wanaidara wote wa idara ya lugha na fasihi kwa maoni na miongozo yao hadi leo nimefanikiwa.

IKISIRI

Utafiti huu unahusu usawiri wa ujinsia katika filamu uchunguzi wa matumizi ya lugha katika filamu za Steven Kanumba. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa kijinsia katika lugha ya filamu za Steven Kanumba ili kuona ni jinsi gani lugha inatumika kusawiri masuala ya kijinsia katika jamii. Utafiti huu ulitumia mbinu nne za ukusanyaji data ambazo ni; maktaba, usaili, dodoso na majadiliano ya vikundi. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya; madhumuni maalum na utuezi nasibu wa sampuli. Utafiti huu umegundua kuwa, filamu za Kanumba zimetumia lugha kwa namna ambayo inasawiri mahusiano ya kijinsia katika jamii mbalimbali hususani jamii ya Watanzania na Afrika. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa Kanumba katika filamu zake ametumia zaidi kejeli na dhihaka kuliko vipengele vingine vya lugha. Matumizi ya kejeli na dhihaka yanaonyesha ndiyo mbinu ya kifani inayotawala kazi za Kanumba. Utafiti huu umedhihirisha kuwepo kwa usawiri wa mwanamke kwa namna mbalimbali. Katika kazi za fasihi za Kanumba imedhihirika kwamba mwanamke anasawiriwa kama mama, chombo cha starehe, kiumbe dhaifu na tegemezi, kiumbe kisichokuwa na maamuzi binafsi, chanzo cha matatizo, msaliti, na ni kiumbe mvumilivu na mnyenyekevu.

Utafiti huu pia umebaini kuwa, matumizi ya lugha katika filamu za Steven Kanumba yanadhihirisha tofauti baina ya mwanamke na mwanaume katika jamii. Imegundulika kuwa kuna mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume. Tofauti ya mahusiano haya imejengeka katika misingi ya kijamii ambapo tangu awali jamii inawaona wanaume ni tofauti na wanawake.

YALIYOMO

ITHIBATI ii

HAKI MILIKI iii

TABARUKU v

SHUKRANI vi

IKISIRI viii

ORODHA YA VIELELEZO xiii

ORODHA YA CHATI xiv

SURA YA KWANZA 1

1.0 UTANGULIZI WA JUMLA 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Tatizo 1

1.3 Tatizo la Utafiti 3

1.3 Lengo la Utafiti 4

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti 4

1.3.2 Malengo Mahususi 4

1.4 Maswali ya Utafiti 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti 5

1.6 Mipaka ya Utafiti 5

1.7 Uzingativu wa Maadili 6

1.8 Matatizo ya Utafiti 10

1.9 Historia ya Kanumba 10

1.9.1 Sehemu Ifuatayo Inaonyesha Kazi Alizofanya 14

1.9.2 Tuzo Alizowahi Kupata 14

1.9.3 Tawasifu ya Kanumba (Kaiandika Mwenyewe) 14
1.10 Muundo wa Tasnifu 17
1.11 Hitimisho 18
SURA YA PILI 19
2.0 MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA 19
2.1 Utangulizi 19
2.2 Historia ya Filamu Afrika 19
2.3 Historia na Maendeleo ya Filamu Nchini Tanzania 21
2.3.1 Filamu Kipindi cha Ukoloni 22
2.3.2 Filamu Baada ya Ukoloni 23
2.4 Tafiti Tangulizi Kuhusu Filamu 26
2.5 Vipengele vya Lugha 27
2.5.1 Tamathali za Semi 27
2.5.2 Sitiari 28
2.5.3 Tashibiha 30
2.5.4 Tashihisi 30
2.5.5 Ishara 31
2.6 Tafiti za Lugha Katika Kazi za Fasihi 31
2.7 Mwega wa Kinadharia 34
2.8 Hitimisho 36
SURA YA TATU 37
3.0 MBINU ZA UTAFITI 37
3.1 Utangulizi 37
3.2 Eneo la Utafiti 37

3.3 Kundi Lengwa 38

3. 4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli...40

3.4.1 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu...40

3.4.2 Uteuzi Nasibu 42

3.7 Utafiti Tangulizi 45

3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data 50

3.7.1 Mbinu ya Maktaba...51

3.7.2 Mbinu ya Usaili 52

3.7.3 Mbinu ya Dodoso 54

3.7.4 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi...55

3.8 Zana za Kukusanyia Data...56

3.9 Uchambuzi wa Data...57

3.10 Hitimisho...58

SURA YA NNE 60

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA 60

4.1 Utangulizi..60

4.2 Muhtasari wa Filamu Zilizofanyiwa Uchunguzi...60

4.2.1 Moses 60

4.2.2 My Valentine..61

4.2.3 Johari...61

4.3 Kubainisha Vipengele vya Lugha Katika Filamu za Kanumba 62

4.4 Mdafao na Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha 62

4.5 Usawiri wa Ujinsia katika Filamu za Kanumba 65

4.6 Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke Katika Filamu za Kanumba 71

4.6.1 Mwanamke Kama Mama 72

4.6.2 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe 74

4.6.3 Mwanamke Kama Kiumbe Dhaifu na Tegemezi 76

4.6.4 Mwanamke Kama Kiumbe Kisichokuwa na Maamuzi Binafsi 78

4.6.5 Mwanamke Kama Chanzo cha Matatizo 79

4.6.5 Mwanamke Kama Msaliti 80

4.6.6 Mwanamke Kama Kiumbe Mvumilivu na Mnyenyekevu 81

4.7 Tofauti ya Mwanamke na Mwanaume Katika Filamu za Kanumba 82

4.8 Hitimisho 84

SURA YA TANO 86

5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 86

5.1 Utangulizi 86

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti 86

5.3 Hitimisho 89

5.4 Mapendekezo 91

MAREJEO 92

VIAMBATISHO 98

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 3.1 Washiriki wa Utafiti..44

Kielelezo 4.1 Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha..............................63

Kielelezo 4.2 Matokeo Kulingana na Jinsi 68

Kielelezo 4.3 Mabadiliko ya Filamu za Kanumba Kuhusu Mwanamke 69

Kielelezo 4.5 Nafasi ya Mwanamke Katika Jamii 71

ORODHA YA CHATI

Chati 4 .1 Mdafao wa Vipengele vya Lugha Katika Filamu za Kanumba 63

Chati 4.2 Matokeo ya Dodoso 67

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Lugha ni mhimili wa kazi yoyote ya sanaa. Watunzi wa kazi za fasihi hutumia lugha inayoambatana na utendaji wa wahusika ili kujenga, kukuza mgogoro baina ya wahusika wa tamthiliya na kupeleka simulio mbele. Sura hii ni sura tangulizi ambayo inabainisha tatizo la utafiti lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu. Sura hii imegawanywa katika sehemu saba. Sehemu ya kwanza inahusu usuli wa tatizo, sehemu ya pili inaelezea tatizo la tafiti, sehemu ya tatu inahusu malengo ya utafiti, sehemu ya nne inahusu maswali ya utafiti ambayo utafiti huu ulikusudia kuyajibu na umuhimu wa utafiti. Sehemu ya tano inajadili vikwazo ambavyo mtafiti alikabiliana navyo wakati wa ukusanyaji wa data za utafiti huu. Aidha, sehemu ya sita ya sura hii inabainisha masuala ya kiitikeli (kimaadili) ambayo mtafiti aliyazingatia kabla, wakati na baada ya kukamilisha zoezi la uksanyaji data za utafiti. Sehemu ya saba inaelezea matokeo ya utafiti wa awali ambao ulifanyika kabla ya utafiti huu kufanyika.

1.2 Usuli wa Tatizo

Tamthilia ni utanzu wa fasihi ambao huwa na majibizano ya wahusika pamoja na vitendo. Kuna tamthilia andishi na simulizi; na hivyo tuseme tamthilia huweza kuwa kipengele cha fasihi andishi na simulizi (Mulokozi, 1996). Katika siku za hivi karibuni tamthilia hizi zimerekodiwa katika filamu na kuuzwa. Moja ya filamu maarufu nchini Tanzania na katika nchi nyingine za Afrika Mashariki ni filamu za Steven Kanumba. Miongoni mwa filamu zake ni pamoja na *Uncle JJ*, *Family Tears*,

Wrong Marriage, *Young Billionaire*, *Moses*, *My Valentine*, *Johari*, *Cross My Sin* na kadhalika. Filamu hizi, zaidi ya mambo mengine, zinatumia lugha ambayo husawiri mambo kadha wa kadha katika jamii. Miongoni mwa mambo hayo ni suala la uongozi, utawala, siasa, jinsia na mambo mengineyo. Utafiti huu unakusudia kuchunguza jinsi lugha inayotumika katika filamu hizo inavyosawiri suala la jinsia.

Fasihi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe kwa hadhira kwa njia ya maandishi ama mdomo na vitendo (Mulokozi, 1996). Kwa kutumia tanzu mbalimbali za fasihi tunaweza kubadili mielekeo, mitazamo, tamaduni, imani, mila na desturi za jamii inayohusika katika muktadha na wakati mahsusi. Fasihi inaweza kutumiwa kuzuia au kuchelewesha maendeleo na mapinduzi. Fasihi inasaidia kujifunza utamaduni wa jamii; kuelewa mwelekeo, itikadi na mahitaji yao, na kuwasaidia kuitumia fasihi yao kuendeleza mazingira yao. Hivyo ni wazi kuwa fasihi huweza kuibua masuala mbalimbali yanayoibuka katika jamii na kuleta athari kwa jamii kwa haraka zaidi (Mulokozi, 1983).

Fasihi ina tanzu nyingi. Mojawapo ya tanzu za fasihi ni ushairi. Ushairi ni utunzi unaotumia lugha ya mkato yenye mnato na mvuto katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii (Mulokozi na Kahigi, 1973). Utafiti huu unachunguza usawiri wa kijinsia katika tamthilia za Kanumba ambazo alitunga ili kuona ni jinsi gani anatumia lugha kuswiri suala la jinsia katika jamii. Aidha kwa kuchunguza matumizi ya lugha katika tamthiliya za Kanumba tutaweza kubaini nafasi ya mwanamke ikilinganishwa na ile ya mwanaume na mahusiano yao katika jamii. Lugha kama zana inayotumiwa na wasanii wa kazi za sanaa katika kufikisha ujumbe kwa jamii huwa na vipengele

mbalimbali vya kiisimu. Vipengele hivi hubeba dhana na ujumbe mbalimbali kwa jamii ambayo msanii amelenga ujumbe huo uifikie. Kwa maana hiyo basi, kama kazi ya fasihi filamu huwa na lengo la kuelimisha, kuonya, kuadilisha na kutunza amali za jamii.

Dhima zote hizi huwasilishwa kwa kutumia lugha ambapo, mtunzi huteua maneno ambayo huyakusudia yalete athari fulani kwa jamii huku yakisawiri mahusiano ya aina mbalimbali baina ya wahusika wa kike na wa kiume kama wawakilishi wa watu wenye sifa mbalimbali katika jamii. Lugha anayopewa mhusika na msanii humsawiri mhusika huyo kama sura ya jamii nzima endapo mhusika huyo atatumiwa na mtunzi kama mhusika jumui. Hivyo basi, utafiti huu utachunguza matumizi ya lugha katika tamthiliya za Kanumba ili kuona ni jinsi namna anavyotumia lugha kusawiri suala ujinsia katika jamii.

1.3 Tatizo la Utafiti

Filamu ni tasnia ambayo imeonyesha kukua kwa kiwango kikubwa na kupendwa na watu wa rika zote nchini na hata nje ya mipaka ya Tanzania. Soko la filamu hizi kwa sasa limekua sana na ni filamu zinazonunuliwa sana kwa sasa. Wasanii wa filamu wanatumia sanaa hii kama njia mojawapo ya kuelimisha jamii, kuonya, kuasa, kukosoa, kuadilisha, kutunza amali za jamii na kueleza hisia na matamanio yao kwa jamii husika. Katika kutimiza dhima hizo, wasanii hao huitumia lugha kisanii ili kujenga maudhui. Lugha inayotumika huwa na dhima kubwa ya kusawiri masuala mbalimbali yakiwemo ya kijinsia. Hata hivyo, kulingana na uelewa wangu hakuna utafiti uliokwisha fanywa kuhusu usawiri wa kijinsia katika lugha inayotumika

katika filamu hizo. Utafiti huu sasa unakusudia kuchunguza matumizi ya lugha katika filamu za Steven Kanumba ili kuona ni namna gani vipengele vya lugha vinatumika kusawiri suala la jinsia na hivyo kuziba pengo lililopo sasa.

1.3 Lengo la Utafiti

Utafiti huu una malengo ya namna mbili, lengo kuu na malengo mahsusi kama inavyofafanuliwa hapa chini:

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa kijinsia katika lugha ya filamu za Steven Kanumba ili kuona ni jinsi gani lugha inatumika kusawiri masuala ya kijinsia katika jamii.

1.3.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu una malengo mahususi matatu.

1. Kubainisha vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba
2. Kujadili sababu za uteuzi wa lugha katika kusawiri masuala ya kijinsia
3. Kujadili jinsi vipengele vya lugha vilivyobainishwa vinavyosawiri mahusiano ya kijinsia baina ya wanawake na wanaume
4. Kujadili nafasi ya mwanamke kama inavyosawiriwa na vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unakusudia kujibu maswali yafuatayo;

1. Ni vipengele vipi vya lugha vinavyotumika katika filamu za Kanumba?
2. Je, ni kwa nini uteuzi wa lugha ya namna fulani hufanyika katika kusawiri masuala ya kijinsia?
3. Je, vipengele vya lugha vilivyobainishwa katika filamu za Kanumba vinasawiri vipi mahusiano ya kijinsia baina ya wanawake na wanaume?
4. Je, nini nafasi ya mwanamke kama inavyosawiriwa na vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu nne; kwanza, utafiti huu unawasaida wanafunzi wa elimu mitindo, wanaisimu na wanafasihi kuelewa jinsi na upekee wa mwandishi katika uteuzi wa vipengele vya lugha kiisimu katika ujenzi wa kazi za fasihi hususani katika tungo za filamu. Pili; utafiti huu utawasaidia wanafunzi na watafiti wengine kupata marejeleo na pia kuwahimiza watafiti kufanya utafiti zaidi katika kazi za fasihi simulizi na andishi hususani katika tasnia ya filamu.Tatu; utafiti huu unatoa mchango katika historia ya filamu na kutoa mchango wa maarifa kuhusu filamu na nafasi yake katika kuelezea mitazamo ya kijamii na hatimaye utatajirisha maktaba ya vyuoni nchini na duniani kote.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza matumizi ya lugha katika filamu za Steven Kanumba zilizotungwa kwa lugha ya Kiswahili. Steven Kanumba ameigiza, kuongoza na kutunga filamu nyingi, hivyo basi, siyo rahisi kuchunguza filamu zote za Steven Kanumba. Kwa maana hiyo utafiti huu ulichunguza filamu ambazo

Kanumba alitunga hadithi ili kuona yeye kama msanii alikuwa na picha gani kuhusu mahusiano ya mwanamke na mwanaume katika jamii. Filamu zilizochunguzwa ni filamu nne tu ambazo ni *Moses*, *My Valentine, She is My Sister v* na *Johari*.

1.7 Uzingativu wa Maadili

Kipengele hiki kinalenga kujadili masuala ya kimaadili yaliyohusika katika utafiti huu na namna mtafiti alivyoweza kuzingatia maadili ya utafiti kabla, wakati na baada ya kukusanya data. Fasili ya utafiti katika fani ya sayansi jamii inasema kwamba ni kitendo kinachohusisha ukusanyaji wa data kutoka kwa watu na wakati mwingine data zinazohusu watu (Padget, 1992; Lee, 1993; Berg, 2004). Hivyo basi, suala la kimaadili katika tafiti za sayansi jamii ni suala ambalo mtafiti hawezi kuliepuka hasa pale anapofanya utafiti wa kitakwimu au usio wa kitakwimu. Kwa mfano, Padget (2004) anabainisha kwamba, masuala ya kimaadili huibuka katika aina zote za utafiti, na utafiti usio wa kitakwimu ukiwemo. Kwa upande wa utafiti huu, ni utafiti wenye sifa za kitakwimu na zisizo za kitakwimu. Hii ina maana kwamba, ni utafiti ambao unatumia mbinu za utafiti wa kitakwimu kwa upande mmoja na usio wa kitakwimu kwa upande mwingine. Hivyo basi, data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili, dodoso, maktaba na majadiliano ya vikundi. Hii ina maana kwamba, kwa kutumia mbinu hizo, utafiti huu ulihusisha makundi ya watu tofauti tofauti, asasi na pia mahusiano ya kibinadamu na tamaduni zao. Kwa maana hiyo, ni dhahiri kwamba, kwa kufanya hivi tusingeweza kuepuka masuala ya kiamaadili na kanuni zake katika kufanya utafiti huu. Daymon na Holloway (2002) wanasisitiza kuwa wakati wa kukusanya data kupitia mahusiano ya kijamii ni muhimu kuweka mkazo wa karibu katika masuala ya kimaadili kwa sababu kuna vipengele

vinayohusiana na mchakato wa kukusanya data. Masuala ya kimaadili ambayo yanapaswa kuzingatiwa katika utafiti ni pamoja na usiri, uwazi, utiifu, ushiriki wa hiari ama kujitolea kwa wahojiwa bila kulazimishwa, kuomba idhini na ruhusa ya kufanya utafiti katika maeneo ya utafiti, na uvumilivu.

Haki za kisheria na vipengele vya kimaadili lazima vizingatiwe katika mbinu zote za utafiti kama ni za kitakwimu au si za kitakwimu (tazama Weiss, 1994; Lofland na Lofland 1995; Silverman, 2005; Belk, 2006). Baada ya kumaliza kuandaa pendekezo la utafiti na kufuata taratibu zote za uwasilishaji wa pendekezo la utafiti katika jopo la kurugenzi ya elimu ya juu, mtafiti alitakiwa kwenda uwandani kukusanya data. Kwa vile utafiti huu ulihusisha watu na asasi mbalimbali, na kwa vile kila asasi ina sheria, taratibu, kanuni na utamaduni wake, mtafiti alihitaji kupata kibali ambacho kilimsaidia kuingia katika maeneo husika. Kibali hiki kilikuwa ni kitu muhimu sana kwa mtafiti ili kuweza kuingia kwenye maeneo ya utafiti.

Suala lingine la kimaadili ambalo mtafiti alisisitiza ni kuwaomba washiriki kushiriki kwa hiari na kujitolea katika kutoa data. Schutt (2006) anasema kuwa, kwa watafiti, ni jambo la muhimu sana kuhakikisha kwamba washiriki wa utafiti wanashiriki kwa kujitolea. Hii ina maana kwamba mtafiti anapaswa kuhakikisha kuwa wahojiwa wanaoshiriki katika kutoa data, watoe data hizo kwa hiari na uamuzi wao binafsi bila kushinikizwa. Hivyo basi, katika mchakato wa kufanya usaili na kugawa dodoso mtafiti alielezea lengo la utafiti kwa washiriki na kuwaomba wajitolee kwa hiari na kushiriki kikamilifu katika usaili na kujibu maswali yaliyopo katika dodoso. Vile vile, wakati wa kutoa maelezo tangulizi ya mwongozo wa maswali ya usaili funge na

dodoso mtafiti aliweka bayana malengo ya shughuli husika. Hali kadhalika, alisisitiza kwamba wahojiwa wanaombwa kujibu maswali ya dodoso na usaili kwa hiari. Aidha, mtafiti alitumia muda huo kujadiliana na wahojiwa juu ya lengo kuu la utafiti huu na matarajio yake ili kupata mawazo, maoni na mtazamo wao. Kwa kuambiwa na kuelewa malengo ya utafiti huu, wahojiwa waliweza kutoa mawazo, maoni na mtazamo wao juu ya kile wanachofahamu kuhusiana na utafiti huu kwa uhuru zaidi. Hivyo basi, kwa kufanya haya, ilisaidia zoezi zima la utafiti na kurahisisha shughuli ya ukusanyaji wa data za utafiti huu.

Jambo lingine la kimaadili ambalo mtafiti alilizingatia ni kuheshimu ridhaa ya washiriki kabla ya kutumia zana za utafiti. Hivyo basi, mbali ya usaili na dodoso, mtafiti alitumia zana za ukusanyaji data kama vile; kinasa sauti, kamera na video kamera. Kabla ya kutumia zana hizi mtafiti aliwaeleza wahojiwa sababu ya kutumia zana hizi na kuwaomba ridhaa yao. Wahojiwa walielezwa umuhimu wa kutumia zana hizo katika utafiti huu, pia walielezwa wazi kuwa kila kitu kitakachorekodiwa pamoja na picha zote zitakuwa ni siri na zitatumika kwa usiri mkubwa kwa ajili ya malengo ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

Wahojiwa walikubali na kuwa tayari kurekodiwa na kupigwa picha za kamera na video ingawa pia wapo baadhi yao ambao walionekana kutoridhika na zoezi hili. Hata hivyo, pale ambapo wahojiwa hawakuwa tayari kurekodiwa mtafiti alilazimika kuandika kila kitu kilichozungumzwa na mhojiwa katika notibuku. Pamoja na hali hiyo, tatizo hili halikuathiri mchakato mzima wa kukusanya data katika utafiti huu. Jambo lingine la kimaadili ambalo mtafiti alilizingatia wakati wa kukusanya data ni

suala la usiri. Kwa kuzingatia usiri inadhihirisha kwamba data za utafiti zitatumika kiasi kwamba hakuna mtu mwingine zaidi ya mtafiti atakaye jua chanzo cha data hizo. Mtafiti lazima ahakikishe kwamba mifano kutoka katika data hazionyeshi wala kubainisha utambulisho wa mshiriki ama mhojiwa. Kwa nyongeza, data zinaweza kuhifadhiwa katika vitu mbalimbali kama vile nyaraka za maandishi, tepurekoda za usaili, tepurekoda za video, na picha. Vitu hivyo vyote vyenye uwezo wa kumtambulisha mhojiwa lazima vihifadhiwe kwa uangalifu wakati wa ukusanyaji wa data na mwishoni mwa utafiti (Silva, 1995; Kvale, 1996; Speziale na Carpenter, 2007; Bachman na Schutt, 2007).

Kwa kuzingatia suala la usiri, mtafiti aliwaahidi na kuwahakikishia wahojiwa walioshiriki katika usaili na kujaza hojaji, kuwa, kila kitu katika data walizozitoa na mjadala wa data hizo utafanywa kwa usiri mkubwa. Wahojiwa hawakutakiwa kuandika majina yao ili kulinda siri ya mtoa data. Hata hivyo, ieleweke kwamba, hakuna urejelezi wa jina uliofanywa katika uchambuzi, uwasilishaji na mjadala wa data. Hata wakati wa mchakato wa kukusanya data mtafiti hakuweza kutoa siri ya data alizopewa na mhojiwa mmoja kwa mhojiwa mwingine, ikiwa ni pamoja na majina yao.

Kulingana na ahadi ambayo mtafiti aliitoa kwa wahojiwa wake, data zote alizokusanya kutokana na rekodi ya usaili, rekodi za video, picha, notibuku, notisi za uwandani na taarifa za hojaji mtafiti amezitunza kwa usiri mkubwa. Hii inaonyesha kwamba mtafiti alichukua hatua muhimu katika kuzingatia vipengele vyote vya uzingativu wa maadili katika utafiti.

1.8 Matatizo ya Utafiti

Katika utafiti huu yapo matatizo ambayo yalijitokeza kabla na baada ya kwenda uwandani. Matatizo, katika utafiti wa aina yoyote ile, hayawezi kuepukika. Hivyo basi si ajabu kwamba katika utafiti huu pia yapo matatizo ambayo yaliyomkabili mtafiti. Matatizo hayo ni pamoja na upungufu wa fedha za utafiti, muda mfupi ambao mtafiti alipaswa kukamilisha utafiti huu, badhi ya watafitiwa kutokuwa tayari kutoa taarifa na ucheleweshwaji wa vibali vya kuendelea na ukusanyaji data. Baadhi ya matatizo hayo kama vile ukosefu wa fedha, watafitiwa kutokuwa tayari kutoa data na ucheleweshwaji wa vibali yalimfanya mtafiti kuchelewa kuanza utafiti wake kama ambavyo alipanga kulingana na ratiba ya utafiti. Aidha, mtafiti alikabiliana na vikwazo hivi kwa kukusanya fedha kwa kunakili data katika shajara na notibuku baada ya kusikiliza tamthiliya za Kanumba. Tatizo la baadhi ya watafitiwa kutokuwa tayari kuhojiwa lilishughulikiwa kwa njia ya usampulishaji nasibu tabakishi ambapo ilichukuliwa kuwa kila memba katika sampuli ya watafitiwa ana nafasi ya kuwa sampuli ya utafiti. Hivyo, mtafitiwa aliygoma kuhojiwa baada ya kuombwa kutoa taarifa za utafiti hakulazimishwa ili kuepusha kutolewa kwa data ambayo isingefaa kwa utafiti huu. Tatitzo la kucheleweshwa kwa vibali vya utafiti lilitatutliwa kwa mtafiti kuongeza masaa ya kukusanya data kwa siku tofauti na alivyokuwa amepanga hapo awali ili kumwezesha kukusanya data ambayo ingekidhi malengo ya utafiti wake.

1.9 Historia ya Kanumba

Steven Charles Kanumba alizaliwa tarehe 8 mwezi wa kwanza mwaka 1984 katika hospitali ya serikali ya mkoa wa Shinyanga mjini Shinyanga nchini Tanzania.

Shinyanga ni eneo ambalo lipo katika kanda ya ziwa. Wenyeji na wakazi wa Shinyanga ni Wasukuma na Wanyantuzu ambao huishi Bariadi. Shinyanga ni moja ya mikoa 21 ya Tanzania bara. Shinyanga wenyeji wake ni Wasukuma, kwa kabila Kanumba alikuwa ni Msukuma, ambapo tunaweza kusema ni Msukuma wa Shinyanga. Tunasema ni Msukuma wa Shinyanga kwa sababu kabila la Wasukuma ni kabila ambalo limechukua Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Hivyo wapo wasukuma wa Mwanza na Wasukuma wa Shinyanga. Kwa asili yake ni kijana wa Kisukuma.

Baba yake anaitwa Charles Kanumba na mama yake anaitwa Flora Mutegoa. Katika historia ya tasnia ya filamu nchini Tanzania, Steven Kanumba ndiye aliyekuwa msanii wa kwanza nchini kufanya kazi nje ya nchi na kuweza kuwavuta wageni kutoka nchi mbalimbali kuja kuigiza Tanzania. Hasa walikuwa Wanaigeria kama vile Mercy Johnson, Emmanuel France, Nkiru Silvanus, Ramsey Nouah, na wengine wengi tu. Kanumba pia ameweza kuwaleta waongozaji filamu kadhaa wa Kinigeria nchini

Kwa kawaida Wasukuma ni wacheshi, wakarimu na wenye upendo na heshima kwa kila mtu. Hizi ni sifa ambazo The Great alikuwa nazo kulingana na marafiki zake, magazeti, vyombo vya habari na televisheni ambazo zilimwelezea Kanumba kwa sifa hizi. Rejea mahojiano ya Janeth mtangazaji wa Televisheni ya Clouds alipohojiwa katika kipindi maalumu kuhusu Kanumba tarehe 7 mwezi wa 4 2012. Alimwelezea Kanumba kama kijana mpole aliyependa kusikiliza na kusaidia kila mtu, kijana mcheshi na mkarimu.

Steven alianza masomo yake katika shule ya msingi ya Buyogi, iliyopo mkoani Shinyanga na baada ya elimu ya msingi alijiunga na shule ya sekondari ya Mwadui. Akiwa kidato cha nne alipata uhamisho na kuhamia katika shule ya sekondari ya Dar Christiana Seminary iliyopo jijini Dar es salaam. Baada ya kuhitimu kidato cha nne Kanumba aliendelea na masomo ya kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari ya Jitegemee iliyopo jijini Dar es salaam. Lugha kuu ambazo alikuwa akiongea ni lugha mama yake ya Kisukuma, Kiswahili pamoja na Kiingereza.

Steven Charles Kanumba alikuwa ni muigizaji na muongozaji wa filamu nchini Tanzania. Alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 28 tarehe 7 April 2012. Inasemekana zaidi ya watu 40, 0000 walihudhuria maziko yake akiwemo mke wa Rais Mama Salma Kikwete, Makamu wa Rais Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wa wakati ule Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi. Steven Kanumba alizikwa katika makuburi ya Kinondoni. Msanii huyu anayesemekana kuwa msanii nyota mkubwa wa filamu nchini Tanzania na pia ndiye msanii aliyeonekana katika filamu za Nollywood.

Kanumba alianza kuigiza katika miaka ya tisini ambapo aliigiza maigizo ya kanisani. Mwaka 2001 alijiunga na kundi la sanaa la Kaole lililopo jijini Dar es salaam. Kwa mara ya kwanza lionekana katika michezo ya kuigiza ya televisheni kupitia michezo ya kuigiza ya Jahazi na Dira. Baadaye alitengeneza filamu yake ya kwanza iliyojulikana kama Haviliki. Mwaka 2006 alionekana katika filamu ya Dar 2 Lagos filamu iliyongozwa na Mtitu Game. Filamu iliyowahusisha wanaigeria na watanzania. Mwaka 2009 alikuwa mgeni maalumu katika mashindano ya Big brother

Africa yaliyofanyika Afrika Kusini. Mwaka 2011 alitangazwa kuwa balozi wa Oxfam GROW. Kabla ya kifo chake alikuwa najiandaa kwenda kuigiza katika filamu za Hollywood.

Kanumba alianza uigizaji miaka ya 90. Katika miaka ya 2002 nyota ya msanii huyu iling'ara na kuwaka katika sanaa ya uigizaji wa filamu ambapo alipata umaarufu mkubwa na kujulikana katika kila kona za nchi ya Tanzania. Kulingana na gazeti la Majira la tarehe 11 mwezi April 2012 katika toleo maalumu Kanumba alifahamika zaidi miaka ya 2002 alipojiunga na kundi la sanaa ya maigizo maarufu kama Kaole Sanaa Group.

Akiwa kama muigizaji aliifanya kama kazi na kitu ambacho alikipenda. Katika mahojiano yake na Clouds TV ya 2012. Alieleza kwamba aliifanya kazi ya uigizaji kama kitu pekee ninachokipenda na kama kazi inayoniingizia kipato. Hivyo basi, Kanumba alipambana kuonyesha kipaji chake na pia kuwaburudisha kuwaelimisha, na kuwaonya watazamaji wake. Filamu alizotunga ni *Johari, Gharika, Baragumu, Sikitiko Langu, Johari 2, Dangerous Desire, Dar 2 Lagosi, Cross My Sin, Village Paster, Family Tears.*

Filamu alizokwisha igiza ni pamoja na; *Jahazi, Dira, Tufani, Gharika, Baragumu, Sikitiko Langu, Johari, Dangerous Desire, Dar 2 Lagosi, Riziki, Cross My Sin* na *The Point of no Return.* Alifanya kazi nyingi ikiwemo uigizaji katika televisheni, uigizaji wa filamu, uongozaji wa filamu, uandishi wa maelezo ya filamu na pia alipata tuzo mbalimbali katika enzi za uhai wake.

1.9.1 Sehemu Ifuatayo Inaonyesha Kazi Alizofanya

Filamu ambazo Kanumba ameshiriki kama mwigizaji ni pamoja na *Haviliki*, *Neno, Ulingo*, *Riziki, Sikitiko Langu, Dangerous Desire*, *My Sister*, *Penina*, *Cross My Sin, A Point Of No Return*, *The Lost Twins, The Stolen Will*, *Village Pastor*, *Magic House*, *Oprah*, *Red Valentine*, *Family Tear*, *The Movie's Director*, *Fake Smile, Unfortunate Love*, *Hero Of The Church*, *Saturday Morning*, *Shauku*, *Crazy Love, 2006 Johari*, *2006 Dar 2 Lagos, 2010 More Than Pain, 2010 Young Billionare, 2010 Uncle JJ, 2010 This Is It, 2010 Off Side, 2011 Deception, 2011 Devil Kingdom, 2011 The Shock,* na *2011 Moses.*

Aidha, Kanumba amewahi kuongoza filamu mbalimbali. Miongoni mwa filamu ambazo ameshiriki katika uongozaji wake ni: *Mr Bahili, Kaka Benny, Lango La Jiji, Papara, Super Model, 2010 Young Billionare, 2010 More Than Pain, 2010 Uncle JJ, 2010 This Is It, 2011 Deception, 2011 Devil Kingdom, 2011 The Shock, 2011 Moses.*

1.9.2 Tuzo Alizowahi Kupata

Vilevile kutokana na kazi za sanaa ambazo Kanumba ameshiriki amepewa tuzo mbambali kutokana na umahiri alioonesha katika kazi hizo. Baadhi ya tuzo alizopata ni: *2006 Best Actor of the Year*, *2007 Best Actor in Tanzania Award* na *2007/2008 Best Artist of the Year Award*. Kanumba alianza uigizaji miaka ya 90.

1.9.3 Tawasifu ya Kanumba (kaiandika mwenyewe)

Kulingana na mtandao wa kijamii facebook Kanumba aliandika profile yake mwenyewe kuhusu yeye alizaliwa wapi na lini na amefanya nini katika maisha yake ya sanaa. Profile hiyo inajionesha kama ifuatavyo;

Steven Charles Kanumba is my name, i was born in a Christian family of 2 girls and i happen to be the last born and the only boy to Mr. & Mrs. Charles Meshark Kanumba.

I was given birth on january 8th 1984. I originate from Shinyanga Region in Tanzania. I am Sukuma by Tribe. I completed my Primary Education in Bugoyi Primary School in Shinyanga. After completing my primary education i started my secondary education right away in Mwadui Seminary Secondary School in Shinyanga where by I shifted to Dar-es-salaam Christian Seminary Secondary school here in Dar-es-salaam when I was still in form II and completed my O-Level Education there. Thereafter I moved to Jitegemee Sec. School to complete my A. Level Education.

Growing up, acting has always been something that I really liked to do. Apart from that i also liked singing and that made me grave to be an artist while I was still in teens, still in school ie. I started acting in church a lot of people told me i had a talent so I decided to join Kaole Sanaa Group which delt with Acting. After joining Kaole Sanaa Group I met different Teachers from Bagamoyo and other College who helped me to build up my career of Acting for a period of 1 year, after that I got a special Training from University of Dar es salaam Under Doctor Nyoni for about 3 months therefore I was sure to go to work and indulge myself in Soap Operas/Series. I then took acting as my career. Little by little I got to win peoples' attention which made me work even harder and become successful.

After all the hard work that I kept in series I decided to play a part in movies so I took a step forward and associate myself in film industry. I happen to do a lot of movies that did very well in the market and I'm still doing movies up today and it just get better day by day. in addition to this I archieved a lot through my hard work that is prestigious awards, travel across different countries, working with people from different part of the world meeting different people and learn new things and experiencing different life.

I also got to get to work with Nollywood in Nigeria where by I did more than five movies with famous actors from Nolllywood, it was the wonderfull experience. I also got a chance to Visit The United States of America and there is where i got the experience of a lifetime I got visit Hollywood, Warner Bros Pictures, Universal Studios and Disney Land, I learnt a lot I met people who work there so I got to ask alot of Quaestions and gained a lot of knowledge.

Speaking about me as Steven Kanumba i'm a very down to earthguy I like hanging out with my friends and I like to associates myself with people, I love children with all my life, I'm just a simple guy, I'm not outgoing a lot, I love going to movies and just be chilled out and relaxed places. I'm not married for the time being but I am in a commitment in the name of God I hope that one day we will get married. I would like to end with my most sincerly appreciation, first and foremost I would like to thank God Almighty for giving and Blessing me a beautiful talent cause apart from acting being my Job, it also happen to be something I love doing and when I am at it I do it with passion.

I would also like to thank my whole family but special appreciation goes to the most beautiful woman in the whole world that happened to be my mother (I Love you Mom) would also like to thank Game 1st Quality Tanzania Limited and again special thank to my brother, my executive Producer and my Advicer Mr. Mtitu G. Game and His Wife. I Would like to thank all the Artist, Producers and Directors I have worked with. Also my special Thanks to my sister Sharifa Kalala in USA and Sanura Hussein in Denmark. Most Importantly, I would lastly like to thank all my fans from different part of the world, thank you all very much for supporting me, I LOVE YOU all and God bless you.Steven Kanumba. Biography hii ni kwamujibu wa tovuti ya www.kanumba.com

1.10 Muundo wa Tasnifu

Tasnifu hii imegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla wa utafiti ambapo masuala yanayohusiana na tatizo lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu yamejadiliwa na kuzingatiwa. Sura ya pili inahusu mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia. Mjadala katika sura hii unaibua pengo la kimaarifa, unajadili mwega wa kinadharia na kufanya mjadala wa kina zaidi juu ya matumizi ya nadharia inayoongoza utafiti huu. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Katika sura hii tunaonyesha mbinu za ukusanyaji data, mbinu za usampulishaji na kujadili mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Sura ya nne ni uchambuzi wa data ambapo data zinawasilishwa, kuchambuliwa na kujadiliwa katika mbinu ya uchambuzi maudhui na mbinu ya uchambuzi linganishi. Sura ya tano, ambayo ndiyo sura ya mwisho, inahusu muhtasari wa matokeo, maoni na mahitimisho ya jumla ya utafiti huu.

1.11 Hitimisho

Sura hii ni sura tangulizi ambayo imejadili juu ya usuli wa tatizo kwa kujadili usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, masuala ya kimaadili na muundo wa tasnifu. Hata hivyo, suala la utafiti linganishi wa kazi za fasihi unajadiliwa kwa undani zaidi katika sura inayofuata ili kuona ni nini kilichokwisha kusemwa na nini hakijasemwa na watafiti wengine kuhusiana na mada hii. Aidha katika sura hii tatizo la utafiti limebainishwa na kuelezwa wazi na kwa undani zaidi. Imeelezwa kuwa lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza usawiri wa kijinsia katika filamu za Kanumba ili kuona ni jinsi gani nafasi ya mwanamke na mwanamume inasawiriwa katika filamu hizo.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandiko mbalimbali kuhusu ujinsia na kuelezea nadharia iliyoongoza utafiti huu. Hivyo, sura hii ina sehemu kuu mbili ambazo ni mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia. Katika sehemu ya kwanza tutafanya mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusiana na filamu na kubainisha pengo la maarifa tunaloliziba. Katika kiunzi cha nadharia tutafafanua nadharia tuliyoiteua, sababu za kuiteua na jinsi ilivyotusaidia katika utafiti wetu.

2.2 Historia ya Filamu Afrika

Barani Afrika sanaa ya filamu ilianza kuonekana kutoka kwa wakoloni, ambao waliitumia kama zana ya kuwaelimishia Waafrika, lakini wakiamini kwamba Waafrika hawakuwa na uwezo wa kutenganisha ukweli na uongo (Diawara, 1992). Mtazamo huu kwa sasa umeshapitwa na wakati, kwani Waafrika wamekwishaelimika kiasi cha kutosha kung'amua mambo mbalimbali yanayoendelea kwenye jamii zao. Kwa ufupi, Waafrika wa sasa wamehamasika tofauti na wale wa miaka ya ukoloni. Pia, si Waafrika wote ambao hawakuweza kutenganisha ukweli na uongo, bali ni mtazamo au kasumba tu iliyojengwa na wakoloni wakati huo ili kuwadharau Waafrika.

Ukadike (1994:1) anaeleza kuwa mwanzoni Waafrika hawakuweza kumiliki filamu mpaka ilipofikia miaka ya 1960 ambapo nchi nyingi za Afrika zilikuwa zikipata

uhuru. Anaendelea kusema kuwa kutokana na wimbi hili la kujipatia uhuru, mataifa ya Afrika kama vile Senegal, Mali, Burkina Faso, Nigeria na Tanzania yalianza kuwa na mamlaka juu ya sanaa hii kwa kutengeneza filamu zao wenyewe. Waandaaji wa filamu wa Afrika walibadili mwenendo wa filamu kutoka ule wa wakoloni ambao ulikuwa na lengo la kuimarisha utawala wa kikoloni na kueneza utamaduni wao. Hivyo wasanii wa Kiafrika wakaanza kuitumia sanaa hii kama chombo muhimu katika mapambano ya kuudumisha utamaduni wa Mwafrika. Walifanya hivi kwa kuchunguza kwa kina utamaduni wa Afrika na kuanza kujenga upya pale ambapo ukoloni ulikuwa umedunisha na kupotosha. Ukadike (1994:166) anaendelea kusema kuwa waandaaji hawa walionyesha hamu ya kuwasiliana na jamii zao, kuamsha uelewa na kisha kuhamasisha jamii zao kupambana na changamoto zinazowakabili.

Cham (1996) anaeleza kwamba, filamu za Kiafrika zimekuwa zikiendana na hali halisi ya jamii za waandaaji wa filamu. Anasema pia kwamba waandaaji hawa wamekuwa wakitumia filamu kama njia ya kusaidia jamii kuondokana na mawazo ya kitumwa, na kukabiliana na changamoto zinazowakabili. Juhudi hizi zinathibitishwa na mwandaaji wa filamu aitwaye Kabore (2000) anaposema kuwa yeye kama msanii ana jukumu la msingi la kuyatilia maanani anayoshiriki, kwa kuwa ana mizizi na historia ambayo imeungana na historia ya jamii yake. Anaongeza kuwa daima anaiakisi hali hii kwenye filamu anazoandaa. Msimamo huo wa Kabore unakuja kipindi ambacho waandaaji wa filamu wanaingiza vionjo vya Kiafrika ili kuyalenga mambo muhimu yanayoendana na maisha ya watu wa jamii husika. Historia hii fupi ya filamu Afrika katika utafiti huu itasaidia katika kutoa picha na kuonyesha maendeleo na malengo halisi ya filamu za Kiafrika. Waandishi waliozungumzia

historia hii wanasisitiza kuwa filamu za Kiafrika zinapaswa kuendana na maisha na hali halisi ya jamii husika ili kuweza kuisaidia jamii hiyo.

2.3 Historia na Maendeleo ya Filamu Nchini Tanzania

Kwa mujibu wa Smyth (1983:129-143), filamu nchini Tanzania ni utanzu wa fasihi ambao ulianzishwa kipindi cha wakoloni. Filamu chache zilizoanzishwa wakati huo zilikuwa na lengo la kuendeleza utawala wa kikoloni na kueneza utamaduni wao. Katika Afrika hakukuwa na sehemu yoyote ambapo palianzishwa kiwanda cha utengenezaji filamu za hadithi ndefu za kifasihi, bali filamu nyingi zilikuwa ni za makala za kuzungumzia matukio halisi. Katika makoloni ya Waingereza, utengenezaji wa filamu za hadithi ndefu umekuwa na mafanikio na kuenea Afrika Magharibi kuliko Afrika ya Kati na Afrika Mashariki. Miongoni mwa sababu zilizokwamisha mafanikio ya utengenezaji wa filamu za kifasihi ni kukosekana kwa mfumo wa kubadilisha fedha za kigeni, udhibiti wa mgawanyo wa fedha hizo na ufinyu wa soko la taifa. Pia kushindwa kwa serikali za Kiafrika kurudisha na kuzitumia fedha zilizopatikana kutokana na kodi ya sinema katika uzalishaji wa ndani wa filamu.

Kwa mujibu wa Nottcut na Lathan (1937), sanaa ya filamu ilianza kuingia nchini Tanzania miaka ya 1920. Kwa upande wa Tanzania maendeleo ya filamu yalichochewa na nchi za Ulaya na za Kiafrika. Mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1920 kulianza kuonekana filamu za Kizungu zilizoletwa na wakoloni kwa lengo la kuimarisha utawala wao katika koloni la Tanganyika. Katika miaka ya 1930 Tanganyika ilichaguliwa kama kituo cha kimataifa cha filamu kilichokuwa chini ya

Wamisheni ambacho kiliitwa BEKE (Bantu Educational Kinema Experiment). Utengenezaji wa filamu katika kipindi cha ukoloni nchini Tanzania, unaweza kuangaliwa kuanzia miaka ya 1933 hadi 1960.

Mponguliana (1982) anaeleza kuwa historia ya filamu Tanzania imegawanyika katika vipindi viwili, yaani wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Vipindi hivi vilitofautiana kulingana na matukio yaliyokuwa yakitokea wakati huo. Kwa mfano, filamu zilizoonyesha harakati za kupigania uhuru zilitengenezwa wakati wa ukoloni. Baada ya ukoloni, filamu zilibeba maudhui yaliyoendana na harakati za Azimio la Arusha. Mgawanyo huu ni muhimu hasa katika utafiti huu kwani unatusaidia kutathmini endapo filamu za sasa pia huakisi kinachotokea katika jamii ya Kitanzania wakati huu. Pia itatusaidia kuonyesha maendeleo ya filamu katika vipindi mbalimbali kama baada ya Azimio la Arusha na wakati wa uchumi au soko huria.

2.3.1 Filamu Kipindi cha Ukoloni

Notcutt na Lathan (1937) wanaeleza kuwa katika kipindi cha ukoloni filamu zilitumika katika mchakato wa kutawala, kuwatia kasumba na kuwapumbaza Watanganyika. Wakoloni walianza kwa kuingiza filamu kutoka nchini Uingereza ambazo ziliakisi mienendo na utamaduni wa kikoloni. Utengenezaji wa filamu Tanganyika ulianza kati ya miaka ya 1935 na 1936 chini ya kampuni iliyojulikana kama *Bantu Educational Cinema Experiment*. Makao yake makuu yalikuwa Vugiri katika milima ya Usambara, Tanga, ambapo mtunzi alikuwa Notcutt na Waingereza wenzie. Filamu nyingi zilizotengenezwa kipindi hiki zililenga kueneza elimu ya kikoloni na kuimarisha ukoloni. Birihanze (1971) katika Jarida la UMMA anaeleza

kuwa katikati ya miaka ya 1960 TANU iliamua kuanzisha Kampuni ya Filamu ya Taifa (TFC). Anasema kwamba hata baada ya kuanzishwa kwa kampuni ya filamu ya taifa hakuna sera zilizowekwa kuhusiana na filamu.

Mponguliana (1982) anaelezea kuwa filamu za mwanzo nchini Tanzania zilitumia lugha ya Kiingereza na maneno machache ya Kiswahili, Kisukuma na lugha nyingine za kikabila. Anaendelea kueleza kuwa utengenezaji wa filamu za kifasihi ulianza Tanganyika miaka ya 1950. Filamu hizi zilizingatia vigezo vya kifasihi kama vile fani, maudhui, maana, muktadha wa kifasihi, na matumizi ya lugha yenye mvuto iliyosheheni tamathali za semi. Baadaye, kampuni ya Afrika Kusini ilipewa jukumu la kutengeneza filamu kwa kutumia mandhari na waigizaji wa Tanganyika na kwa lugha ya Kiswahili katika mikoa ya Dar es salaam na Dodoma.

2.3.2 Filamu Baada ya Ukoloni

Kipindi hiki kinaanzia mwaka 1961, yaani baada ya Tanganyika kupata uhuru, na kuendelea mpaka miaka ya 1990. Toka kipindi hicho kumekuwa na mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za maisha kama siasa, utamaduni, hali ya uchumi, na mtindo wa maisha ya watu kwa ujumla. Hali hii imeathiri kazi mbalimbali za fasihi kwa kuzifanya ziwe na sura mbalimbali. Mponguliana (1982) na Mwakalinga (2003) wanaelezea kuwa katika miaka ya 1960 kulikuwa na jitihada za awali za kufufua tasnia ya filamu nchini Tanzania. Katika kufanikisha hilo mwaka 1963 ilianzishwa Kampuni ya Filamu ya Taifa (NFC) iliyokuwa na jukumu la kusimamia maadili katika utengenezaji wa filamu, na shughuli nzima ya uendeshaji wa filamu nchini Tanzania.

Mwaka 1964 wataalamu wa filamu kutoka Yugoslavia walifika Tanzania kupanga upya masuala ya filamu. NFC ilisaidia katika kutengeneza filamu za makala simulizi zilizoelezea mambo halisi kutegemeana na matukio maalumu kama vile ziara za kitaifa, gwaride na shughuli nyingine muhimu. Kati ya filamu hizo ni *Tanganyika Triumphant* (1962), *Road Ahead* (1963) na *The Land of Promise* (1963).

Kwa sasa, filamu hizi zinatumika katika kuonyesha kumbukumbu za matukio ya kitaifa kama vile Siku ya Uhuru. Wakati wa Azimio la Arusha filamu ilikuwa chombo muhimu katika kutangaza sera za Ujamaa na Kujitegemea, na Vijiji vya Ujamaa. Wakati huo TANU ilikuwa mstari wa mbele katika kuendeleza filamu nchini Tanzania. Filamu wakati wa sera ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea zililengwa kuonyesha masuala kama vijiji vya ujamaa, elimu ya kujitegemea na ukombozi. Kwa ufupi, filamu zilizotolewa wakati wa Azimio la Arusha zilihamasisha harakati za ukombozi. Lakini, kwa upande mwingine, mabepari waliokuwepo wakati ule walitumia filamu na televisheni kama chombo cha kutekeleza matakwa ya ubepari, urasimu na propaganda.

Kulikuwa na juhudi za kuwachanganya Watanganyika kwa kuwaonyesha filamu za Kizungu ambazo hazikuwa na uhusiano na mambo yaliyokuwa yanatokea kwenye jamii ya Kitanganyika. Walitumia filamu kupinga itikadi ya kijamaa ili kuwanyima au kuwanyang'anya Watanganyika ari ya kuzitazama filamu zilizolenga kuusimika ujamaa na kuhamasisha ukombozi. Filamu nyingi zilizoingizwa Tanganyika wakati ule zilikuwa za Kizungu na zilitengenezwa kwa ajili ya soko la Marekani. Mfano wa filamu hizo za kibepari ni kama vile *Hammer* na *Slaughter*. Wahusika na mandhari

iliyotumika katika filamu hizi ilikuwa ni ya Kizungu. Mathalani, katika filamu ya *Slaughter,* kulikuwa na wahusika Jim Brown na ex-Green Beret ambao walikuwa askari wa kibepari wa Marekani. Filamu hizi zilioonyesha matukio ya vurugu, ngono, matukio ya kikatili na makosa ya jinai kama mauaji. Hii iliwafanya Watanganyika, na Waafrika kwa ujumla kuwa na woga katika harakati za ukombozi za kupigania haki zao Birihanze (1971:43) katika Jarida la UMMA.

Mponguliana (1982) anaeleza kuwa filamu zilizochezwa na wasanii wa Kitanganyika zilianza kuonekana kati ya miaka ya 1960 na 1970. Filamu ya kwanza inayojulikana kama *Muhogo Mchungu* ilitoka miaka hiyo na ilichezwa na Rashid Mfaume Kawawa ambaye kwa wakati huo alikuwa miongoni mwa viongozi wa nchi. Rashid Mfaume Kawawa, alichukua uhusika na kucheza kama wahusika wengine. Hii ilifuatiwa na *Fimbo ya Mnyonge* iliyotoka mwaka 1974. *Harusi ya Mariam* pamoja na *Yomba Yomba* zilitoka mwaka 1983. Kutazama mapitio haya ya historia ya filamu Tanzania kutasaidia kuonyesha jinsi tasnia ya filamu ilivyopiga hatua, na kuonesha inakoelekea.

Kuanzia miaka ya 1980, kumekuwa na kushamiri kwa tasnia ya filamu kutokana na mfumo wa soko huria. Katika kipindi cha soko huria yaani kuanzia miaka ya 1990 kulikuwa na uhuru wa kuanzisha makampuni binafsi ya habari na kazi mbalimbali za sanaa. Mfumo wa soko huria ulichochea makampuni binafsi kuwa na mwamko wa kufadhili filamu zilizokuwa na dhumuni la kuelimisha watu/ jamii katika nyanja mbalimbali kama masuala ya kijamii na ya kiuchumi. Kushamiri kwa tasnia filamu kumeendelea mpaka miaka ya karibuni yaani miaka ya 2000 na ambapo soko la

filamu limechukua sura mapya na limepiga hatua kwa kuwa na wasanii wengi (Kabore, 2003: 171).

2.4 Tafiti Tangulizi Kuhusu Filamu

Watafiti mbalimbali wamefanya tafiti kuhusu filamu nchini Tanzania. Mponguliana (1982) alifuatilia maendeleo ya filamu Tanzania. Yeye alijikita kwenye utengenezaji wa filamu katika kipindi kabla ya ukoloni, baada ya ukoloni na baada ya uhuru. Utafiti uliofanywa na Mponguliana umesaidia katika utafiti huu kwa kuonyesha maendeleo ya sanaa ya filamu nchini Tanzania hususan vipindi mbalimbali ambavyo tasnia hii imepitia.

Mwakalinga (2003) amezungumzia nafasi ya mwanamke katika filamu za Kitanzania. Anaeleza kwamba wanawake wanastahili kusawiriwa katika mtazamo chanya ili kuwasilisha picha sahihi ya wanawake wa Kiafrika. Wanawake pia wanatakiwa kuandika hadithi zao wenyewe, na kutengeneza na kusimamia filamu zao wenyewe. Utafiti wa Mwakalinga unasaidia kuonyesha jinsi ambavyo filamu za Kitanzania zimekuwa zikisawiri wanawake na mambo yanayotokea kwenye jamii. Unasaidia pia katika kuchambua nafasi mbalimbali za mwanamke katika filamu za *Taswira* na *Vita vya Ushindi.*

Shule (2004) amefanya utafiti juu ya mchango wa filamu katika harakati za kupunguza unyanyasaji wa kijinsia na hatari zinazoweza kusababisha UKIMWI. Katika utafiti wake ameonyesha jinsi filamu zinavyoweza kusaidia kuwaelimisha vijana wa kiume katika kuzuia unyanyasaji wa kijinsia ambao ni mojawapo ya

mambo yanayoweza kusababisha kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI. Stadi hii inatoa mwanga juu ya mambo au majanga ya jamii yanavyoweza kuingizwa kwenye filamu na kutumika kama njia ya kuifundisha au kuikanya jamii.

Njewele (2007) yeye ametazama jinsi maonyesho ya kitamaduni yanavyotumiwa kwenye filamu za Kiafrika. Anaona kwamba filamu chache sana zinaonyesha maonyesho ya kitamaduni ya Mwafrika. Anataja mifano ya filamu hizo kama *Harusi ya Mariamu* (1985) na *Maangamizi* (1998). Anapendekeza kuwa watengenezaji wa filamu wazingatie maonyesho ya kitamaduni ya Kiafrika katika filamu zao ili kuyahifadhi kwa ajili ya utambulisho na manufaa ya kizazi kijacho. Kwa kuzingatia hili, filamu inaweza kuonyesha au kutambulisha taifa fulani kwa kuangalia yale yanayoonyeshwa hasa kwa kuzingatia utamaduni wa jamii husika. Utafiti wa Njewele unasaidia katika uchambuzi wa masuala ya kitamaduni yanayojitokeza katika filamu za *Taswira* na *Vita vya Ushindi.*

2.5 Vipengele vya Lugha

Lugha ina vipengele mbalimbali ambavyo hutumiwa katika kazi za fasihi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyo kusudiwa. Moja ya kipengele cha lugha ni tamathali za usemi. Hivyo katika utafiti huu tutachunguza vipengele vya lugha ambavyo vimejikita katika uhamishaji wa maana kutoka katika dhana moja kwenda katika dhana nyingine ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.

2.5.1 Tamathali za Semi

Tamathali za semi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza,au kubadilisha

maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi. (Mulokozi na Kahigi (1979) tamathali zinazotumika zaidi katika ushairi ni tashibiha, tashihisi, kejeli, matonimia na sitiari.

Kahigi (1994) anadi kuwa msingi wa tamathali za semi nyingi ni uhamishaji wa maana. Uhamishaji wa maana ni mbinu ya kuibua maana ya kiashiria (neno, fungu n.k) kutokana na maana ya kiashiria kingine. Kanuni ya jumla ya uhamishaji wa maana ni maana ya kitamathali X inachukua nafasi ya maana ya kawaida Y iwapo X inahusiana na Y kwa njia fulani. Tamathali za semi ambazo zinahusika na uhamishaji wa maana ni kama ifutavyo;

2.5.2 Sitiari

Ni uhamishaji wa maana toka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vikoa vya maana vinavyohusika katika uhamishaji huu huwa vinatofautiana angalau kwa sifa ya kisemantiki moja ya msingi. Kinachohamishwa ni tabia au umbo au kazi ya kitu kwa kuihusiha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine. Mfano katika kipande cha wimbo huu;

Mama yangu wewe ni nguzo maishani mwangu
ni taa imulikayo mbele yangu
mawazo yako mamaa yaniongoza maisha yangu yooote.

Hapa hatumanishi kuwa mama amegeuka kuwa nguzo au taa bali kinachohamishwa ni zile sifa za nguzo na taa zinahamishiwa kwa mama. Yaani, nguzo ina sifa ya kutoa

msaada, mtu anapoegema au kushikiria nguzo humpa msaada. Taa huto mwanga, humulika giza na kuleta nuru. Hivyo sitiari taa na nguzo zimetumika kuonesha umuhimu wa mama katika malezi ya mtoto.

Muundo wa sitiari una vipengele vitatu: kizungumzwa, kifananisho na kiungo (Lakoff & Johnson (1988); Kahigi (1994). Kizungumzwa ni kitajwa, ambapo katika mfano wetu ni mama, kifananishi ni kitu kinachohusishwa na kizungumzwa hapa ni taa na nguzo, kifananishi ni tabia au sifa zinazounganisha kizungumzwa na kifananishi hapa ni msaada, mwanga/nuru.

Kimsingi kuna sitiari za aina tatu; sitiari pana, changamano na sahili (Kahigi, 1994). Kahigi pia anafafanua sitiari hizo kuwa; sitiari sahili ni sitiari ya moja kwa moja na ina kifananishi kimoja, sitiari chanagamano huwa na vifannaishi viwili au zaidi vinavyochangia kutoa dhana mbalimbali juu ya kizungumzwa. Sitiari pana ni ile inayojengwa na semi nyingi za kisitiari na inaweza kuwa sehemu ya shairi, hadithi au tamthiliya au inaweza kuwa msingi na kiunzi cha muundo wote wa shairi, hadithi, au tamthiliya.

Hivyo sitiari hutumika katika kazi za fasihi ili kujenga maana na ujumbe katika jamii. Katika kazi za fasihi wasanii hutumia kipengele cha sitiari ili kuibua maana na ujumbe. Matumizi ya sitiari hutegemea na wakati na muktadha wa utumizi. Sitiari moja inaweza kuashiria maana zaidi ya moja katika muktadha na wakati fulani mfano ngoma huweza kuashiria ukimwi katika muktadha wa ugonjwa na pia huweza kuashiria mwanamke katika muktadha wa mapenzi. Vile vile sitiari zaidi ya moja

huweza kubeba maana moja mfano ngoma, umeme, miwaya, zote huashiria ukimwi (Jilala, 2008)

2.5.3 Tashibiha

Kahigi (1994) anafasili tashibiha kuwa ni usemi wa kimlinganisho utumiao maneno kama mithili ya, kama kwamba, n.k kwa mfano mweusi kama mkaa, mweupe mithili ya theluji n.k. naye Senkoro (1982) anafasili tashibiha kuwa ni tamathari ambayo watu ama vitu viwili au zaidi hulinganishwa na watu ama vitu vingine kwa kutumia maneno kama, mithili, kama kwamba, mfano wa, na mengine ya aina hiyo. Mfano bwana Msa ni mweusi kama mkaa. Hivyo hapa tashibiha imetumika kulinganisha rangi ya bwana Msa na mkaa. Dhana hii ya ulinganishaji hutumika kuonesha tabia, sifa zinazolinganishwa hivyo weusi wa bwana Msa unalinganishwa na mkaa.

Ukitazama fasili hizo utaona kuwa wataalamu hao wanakubaliana kwa pamoja kuwa tashibiha hulinganisha vitu ama watu kwa kutumia maneno kama vile mithili ya, kama, mfano wa n.k.

2.5.4 Tashihisi

Senkoro (1982) anafasili tashihisi kuwa ni tamathali ya usemi ambayo wakati mwingine huitwa fasili ya binadamu. Kwa tamathali hii vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo. Mfano nyota zilikuwa zikitabasamu huku zimemzunguka mama yao. Usiku uliukumbatia ulimwengu kwa kumbato la kutisha la giza nene na kimya kingi. Sambamba na Senkoro, Kahigi (1994) anafasili tashihisi kuwa ni usemi ambao sifa ya uhai huwa imehamishiwa kwenye kitu kisicho na uhai

au dhana dhahania (pengine tashihisi hiuitwa uhaishaji) tashihisi hutumiwa zaidi na washairi ambao kwa mfano hawasiti kusema kimya hakishi kunenea, kitakapo kusimamia, fedha huita wazuri wakaitika labeka, maji baridi yaliubusu mwili wake mwororo. Katika mifano hii kimya kimepewa sifa ya kibinadamu ya kunenea na kusimamia, fedha imepewa sifa ya kuita na maji yamepewa sifa ya kubusu.

Hivyo basi, ukichunguza mifano hiyo utaona kuwa tashihisi hutumika kwa kuvipa vitu visivyo na uhai uhai na uwezo wa kutenda kama binadamu. Mfano nyota zimepewa uwezo wa kutabasamu na kutenda kitendo cha kumzunguka mama yao, aidha usiku nao umepewa uwezo wa kutenda kama binadamu hivyo usiku nao umepewa uhai.

2.5.5 Ishara

Ni neno au usemi wenye maana inayowakilisha dhana nyingine kwa kuhusiana nayo. Yaani neno,au usemi huo huwa na viwango viwili vya maana. Maana ya moja kwa moja na maana ya kitamathali. Ishara inaweza kuwa na msingi wa kisitiari kama taa mwenge ambayo hutumika kuwakilisha utambuzi, ujuzi n.k au inaweza kuwa na msingi wa kitaashira kama kaburi, jeneza, fuvu ambayo hutumika kuwakilisha mauti (kahigi 1994).

2.6 Tafiti za Lugha Katika Kazi za Fasihi

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu vipengele vya lugha katika kazi za fasihi. Tafiti hizo zinajikita katika fasihi andishi na fasihi simulizi. Kazi zinazoangaliwa zinazojadiliwa hapa ni kazi ya Ligembe (1995), Mosha (2002) na Ramadhani (2005) na Jilala (2008). Ligembe (1995) amechambua matumizi ya sitiari katika kazi ya ya

Lina ubani iliyoandikwa na Penina Muhando. Katika uchunguzi wake amejadili muundo na umbo la tamthiliya ya Kiswahili. Amebainisha kiungo, kifananishi na kizungumzwa na kuelezea mchango wake katika uelewa wa tamthiliya. Tofauti na watafiti wengine Ligembe (keshatajwa) amejikita zaidi katika umbo la tamthiliya ya Kiswahili na kubinisha aina za sitiari. Utafiti wake haukuonesha uhusianao uliopo baina ya aina ya sitiari na ujenzi wa dhamira katika tamthiliya.

Ramadhani (2005) alifanya utafiti wa matumizi ya sitiari katika tamthiliya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein na *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ya Emmanuel Mbogo. Utafiti ni utafiti linganishi wa kielimumitindo ambapo analinganisha tamthiliya mbili. Aidha katika ulinganishi hakuwa mbali na hitimisho la Mosha kuwa sitiari sahili ndiyo yenye mdafao mkubwa kuliko sitiari zingine katika tamthiliya zote. Aidha alihitimisha kuwa sitiari hutumika katika ujenzi wa dhamira mbalimbali katika tamthiliay zote mbili.

Omari (2006) aliandika makala juu ya mitindo na matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya Tanzania. Katika makala hii amebainisha jinsi wasanii muziki wa kizazi kipya wanavyoitumia lugha katika kazi zao. Amebainisha matumizi ya lugha ya majigambo, nyimbo za watoto, kuchanganya lugha, lafudhi mbalimbali, taswira, misimu au misemo, tashihisi, lugha isotafsida, tanakali sauti, methali, takriri, sitiari, tashibiha na utohoaji wa maneno. Hivyo katika makala hii hakuonesha ni jinsi gani lugha inatumika katika ujenzi wa maana, ujumbe na dhamira za kazi za fasihi hivyo makala hii imebainisha vipengele vya lugha vinavyotumika katika muziki wa kizazi kipya.

Jilala (2008) alifanya utafiti juu ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya kwa kuchunguza jinsi wasanii wanavyotumia sitiari kisanii katika ujenzi wa maana na ujumbe. Katika utafiti wake alihitimisha kuwa sitiari pana ndiyo yenye mdafao mkubwa zaidi ya sitiari sahiri na changamano. Hii ni kwa sababu nyimbo za kizazi kipya hutumia vipengele vya lugha kisanii katika kujenga maana na ujumbe. Aidha anaongeza kuwa sitiari hutumika katika kujenga maana na ujumbe na vilevile dhamira mbali mbali katika kazi za fasihi huibuliwa kutokana na sitiari iliyotumika. Jilala anaendelea kusema kuwa muktadha wa utumizi, uzoefu, maarifa na ujuzi na utamaduni wa jamii iliyomlea msanii na hadhira yake ndiyo huongoza katika tafsiri ya maana ya sitiari na ubunaji wa kazi ya fasihi. Katika tasnifu hii Jilala alionyesha nafasi ya mwanamke na namna wasanii wa muziki wa kizazi kipya wanavyomchora mwanamke na nafasi yake katika jamii. Anaeleza kuwa mwanamke huchorwa kama chombo cha kumstrehesha mwanaume, chanzo cha matatizo na pia ni kiumbe tegemezi asiye na maamuzi binafsi, ambaye hawezi kusimama bila mwanaume. Tofauti na utafiti wa Jilala, utafiti huu unachunguza kwa kina nafasi ya mwanamke hususani katika filamu ili kuona ni jinsi gani filamu zinatumika kuelezea suala la ujinsia katika jamii. Na kuonyesha tofauti ya mwanamume na mwanamke.

Jilala (2010/2011) katika makala yake ya lugha na ujinsia katika ushairi ambapo alifanya uchunguzi wa sitiari za UKIMWI na mapenzi katika mashairi ya Bongo fleva anajadili kuwa katika mashairi ya Bongo fleva sitiari zinazomrejelea mwanamke zimebeba dhana tano ambazo zimeundwa kitaswira kumuashiria mwanamke na nafasi yake katika jamii. Dhana hizo ni thamani, unyenyekevu, utamu na mvuto. Tofauti na sitiari zinazomwelezea mwanamume ambazo hubeba taswira ya

uhodari, ushujaa na mwenye maamuzi binafsi. Jilala alichunguza kipengele kimoja tu cha lugha bongo fleva tofauti na utafiti huu ambao utachunguza suala la ujinsia katika filamu ili kuona nafasi ya filamu katika kujadili suala la ujinsia katika jamii.

Ukichunguza tafiti zilizofanywa utaona kuwa ni dhahiri kuwa kazi nyingi zimejikita katika kipengele kimoja cha lugha na pia kujikita katika tanzu zingine na si filamu. Hivyo basi utafiti huu unachunguza kwa kina matumizi ya vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba ili kuona ni jinsi gani lugha inatumika katika kusawiri masuala ya kijinsia katika jamii.

2.7 Mwega wa Kinadharia

Kuna nadharia mbalimbali ambazo hutumika kuchambua lugha katika kazi za fasihi. Makala hii inatumia nadharia ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike (*Feminist Psychoanalytic Theory*). Hii ni nadharia iliyoibuka kutokana na kazi zilizoasisiwa na Jacques Lacan kama alivyonukuliwwa na Momanyi (2001). Nadharia hii inahakiki matini katika misingi ya uchanganuzi nafsia. Huzingatia kuweko kwa nafsi bandia au nafsi isiyo halisi iliyojengwa kutokana na mielekeo ya kiuana, utaratibu fiche wa kisaikolojia pamoja na taasubi za kiume.

Katika utaratibu fiche, maumbo halisi ya kiisimu katika akili ya mwanamke hughubikwa na badala yake maumbo ya kidhahania huimarishwa. Maumbo haya yasiyo na uhusiano wowote na uhalisia wake kama binadamu ndiyo yanayobainika hususan kupitia lugha na tabia yake. Utaratibu huu ambao ni wa kiishara ndio unaoashiria tofauti za kiuana zinazopatikana katika utamaduni wa jamii.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, nafasi ya mwanamke imefungamana na lugha inayomzungumzia, lugha inayoashiria uanawake. Nafasi hii hufinyangwa na jamii kupitia asasi mbalimbali ili aweze kukubalika katika utaratibu huo wa kiishara. Uchanganuzi nafsia katika mtazamo wa kike basi, ni nadharia bia ya uumbaji wa nafsi katika misingi ya uana.

Sababu ya kuteua nadharia hii, ni kwamba wapo watafiti ambao pia wametumia nadharia hii katika kuchambua mahusiano ya mwanamke na mwanamume katika kazi za fasihi mfano Momanyi (2001) na iliweza kuwafikisha kwenye mafanikio katika kuibua suala la ujinsia katika fasihi. Vilevile tumetumia nadharia hii kwa kuzingatia uwezo wake wa kuonesha mahusiano ya kijinsia baina ya wanaume na wanawake katika jamii. Mahusiano na mgawanyo wa majukumu kijinsia katika jamii mbalimbali hujidhihirisha wazi kwa kuzingatia lugha inayotumiwa na wanajamii wakati wanapowasiliana. Kwa kuzingatia msingi huu ndio maana tumetumia Nadharia ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike. Hivyo nadharia hii inaweza kutumika katika kuchambua ujinsi suala la ujinsia linavyosawiriwa na kwa kuzingatia lugha iliyotumiwa katika tamthiliya za Kanumba zilizoteuliwa katika utafiti huu.

Katika muktadha wa uchambuzi wa tamthiliya za Kanumba, nadharia hii inaweza kutumiwa kwa kuzingatia kwamba lugha haiwakilishi uhalisia bali ni utaratibu wa kiishara. Hivyo taswira za wanawake katika fasihi aghalabu haziwakilishi uhalisi wao bali ni taswira bandia zilizosheheni ishara za uana, hususani katika matumizi ya lugha. Aidha uhakiki huo una wajibu wa kuzingatia kuwepo kwa taasubi za kiume

zilizoimarishwa ndani ya utaratibu wa kiishara katika mfumo wa kuumeni. Taasubi hizo ndizo zinazomdunisha mwanamke na kumweka katika kitengo maalumu kijamii (Momanyi, (2001). Nadharia hii itatumika pia kujadili jinsi lugha ya kiishara inavyotumika kuonesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanamume katika jamii.

Kwa kutumia nadharia hii tutaonesha jinsi gani mwanamke anavyochorwa kiishara kwa kutumia lugha. Aidha tutajadili namna ishara ambazo zinaibuka kutokana na lugha iliyotumika katika filamu teule ili kusawiri suala la kijinsia katika jamii.

2.8 Hitimisho

Katika sura hii tumewasilisha mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada tunayoishughulikia na kiunzi cha nadharia. Tumebainisha kuwa kati ya maandiko yote tuliyopitia hakuna andiko hata moja ambalo linashughulikia lugha ya filamu na usawiri wa jinsia. Aidha tumebainisha kuwa utafiti huu unatumia nadharia ya uchangunuzi nafsia kwa kuzingatia mtazamo kike kama ilivyojadiliwa na wataalamu mbalimbali.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inajadili juu ya mkabala wa utafiti, mbinu, na vifaa ambavyo vilitumika katika utafiti huu. Kwa vile utafiti huu ulilenga kuchunguza athari za kiutamaduni katika tafsiri, kubainisha vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba, kujadili ujinsia katika filamu hizo, mtafiti alitumia mkabala wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika kukusanya na kuzichambua data za utafiti huu. Kama wanavyoeleza (Kombo na Tromp, 2006) kuwa, utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu hujazilizana na kukamilishana. Kwa maana hiyo utafiti huu utahusisha maelezo ya data na pia utatumia nduni za utafiti wa kitakwimu kama vile matumizi ya namba na asilimi kuelezea matokeo ya data za usaili na dodoso. Hivyo basi, sura hii inajadili masuala ya methodolojia ya utafiti kwa njia zote mbili yaani; njia ya kitakwimu na isiyo ya kitakwimu ili kujadili, kuchambua na kuonyesha ni jinsi gani matokeo ya utafiti na yameweza kufikiwa.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika nchini Tanzania katika jiji la Dar es Salaam. Sababu ya kuteua jiji la Dar es Salaamu kuwa ndiyo eneo la utafiti kwanza ni uwepo makampuni ya wasambazaji, uzalishaji na watengenezaji wa filamu ambapo filamu za Kanumba zilitengenezwa katika makapuni hayo. Vile vile kuwepo kwa kampuni ya *Kanumba The Great* na watu aliofanya nao kazi ikiwa ni pamoja na waigizaji na wafanyakazi wengine. Hivyo kwa sababu hizo utafiti huu uliona itakuwa rahisi kupata data za kutosha kuhusu utafiti huu na pia upatikanaji wa waigizaji wa filamu ambao asilimia

kubwa ya waigizaji nyota wa filamu ambao walifanya kazi zao na Kanumba wanaishi na kufanyia kazi zao Dar es salaam. Aidha Dar es Salaamu ilikuwa na umuhimu kwa sababu ya kuwepo kwa Chuo kikuu cha Dar es Salaamu ambapo mtafiti alitegemea kuwahusisha wanafunzi wanaosoma kozi za fasihi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaamu.

3.3 Kundi Lengwa

Kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti (Kothari, 2004; Bryman, 2004; Kombo na Tromp, 2006). Walengwa waliohusishwa katika utafiti huu ni pamoja na waongozaji na waandaaji wa filamu za Kanumba, wasanii (watendaji ama waigizaji katika filamu za Steven Kanumba), hadhira (ambao ni watumiaji, mashabiki, watazamaji na wasikilizaji wa filamu za Steven Kanumba), wanafunzi wa uigizaji na filamu (ambao wana maarifa ya fasihi na uchambuzi wa fasihi katika nadharia na vitendo). Hivyo basi, utafiti huu uliliona kundi hili kuwa ndilo lenye uwezo wa kutoa data juu ya filamu za kanumba na suala la ujinsia.

Kwa upande mwingine, sambamba na wao waandaaji, waigizaji, hadhira na wanafunzi wa ugizaji na filamu walionekana kuwa ni watu muhimu katika utafiti huu kwa sababu kwa kuwatumia ilikuwa rahisi kupata data kutoka kwa watu wenye maarifa na uzoefu katika kutumia mbinu, nadharia na vitendo katika filamu na uigizaji. Hadhira ya filamu za Kanumba ilionekana muhimu kwa sababu wao ndiyo watazamaji wa filamu za kanumba na ni mashabiki wa filamu hizo. Hivyo basi, walikuwa na uwezo wa kuelezea juu ya kile ambacho wanakielewa katika filamu za Kanumba na mtazamo na hisia zao juu ya filamu hizo katika suala zima la jinsia.

Kwa upande mwingine wanafunzi wa filamu na uigizaji walionekana kuwa na umuhimu mkubwa sana katika utafiti huu kwa sababu wao ndio wenye maarifa juu ya nadharia na mbinu katika uigizaji na filamu. Hivyo ilikuwa rahisi kwao kutoa data za kutosha kuhusiana na filamu za Kanumba na namna zinavyosawiri suala la ujinsia katika jamii.

Hivyo basi mtafiti aliwahusisha waongozaji wa filamu, wasanii wa filamu na hadhira ya filamu. Waongozaji wa filamu waliteuliwa kwa sababu ndio wanaoongoza filamu hivyo walionekana kuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu. Wasanii wa filamu waliteuliwa kwa sababu ndio walioshiriki katika kuigiza filamu za Kanumba hivyo katika utafiti huu walionekana kuwa na maarifa ambayo yangetosheleza data za utafiti huu.

Aidha, hadhira ya filamu iliteuliwa kwa vigezo kwamba hawa ndio watazamaji na mwashabiki wa filamu za Kanumba. Hivyo basi, utafiti huu uliamini kuwa kwa kuwahusisha hadhira ya filamu tuliweza kupata data za kutosha kuhusu mtazamo wao juu ya suala la ujinsia katika filamu za Kanumba. Hivyo basi, maswali ya dodoso na usaili yalilenga kuchunguza suala la ujinsia katika filamu za kanumba na namna vipengele vya lugha vinavyotumika katika kujenga mtazamo wa jamii juu ya ujinsia katika filamu za kanumba.

Kwa upande mwingine, utafiti huu ulifanyika katika chuo kikuu cha Dar es Salaam ambako wanafunzi wa filamu na uigizaji katika chuo kikuu cha Dar es Salaam walihusishwa ili kubaini mchomozo wa vipengele vya lugha katka filamu za kanumba kutoa maana za maneno yaliyohusishwa katika filamu za Kanumba.

3. 4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli, kama unavyoelezwa na Bryman (2004), ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Zipo mbinu mbalimbali za uteuzi wa sampuli lakini sampuli ya utafiti huu itateuliwa kwa kutumia njia mbili, yaani *uteuzi wa madhumuni maalumu* na *uteuzi nasibu*. Kama ilivyokwisha elezwa kuwa utafiti huu unatumia mkabala wa utafiti usio wa kitakwimu na utafiti wa kitakwimu. Hivyo matumizi ya mbinu hizi mbili za uteuzi wa sampuli yalikuwa na umuhimu mkubwa ili kufikia malengo ya utafiti huu. Maelezo ya mbinu zilioztumika katika uteuzi wa sampuli ya utafiti huu kutoka katika kundi lengwa lililobainishwa na kuelezewa katika sehemu namba 3.2 zinajadiliwa katika vipengele vifuatavyo hapa chini.

3.4.1 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu

Mtafiti alitumia mbinu yenye madhumuni maalumu kuteua sampuli ya utafiti huu. Uteuzi sampuli kwa kigezo cha madhumuni maalumu ni uteuzi wa sampuli kwa kuzingatia sababu mahsusi. Kombo na Tromp (2006) wanasema, ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu ambao anaamini kuwa ni raslimali anayoitegemea katika utafiti wake. Kwa hiyo mbinu hii ilikuwa bora na ya muhimu katika utafiti huu kwa sababu baadhi ya watu katika kundi lengwa walikuwa na uwezo na ni raslimali kubwa katika data za utafiti huu kulikoni wengine. Kwa mfano suala la kiwango cha ufahamu wa nadharia na mbinu katika utunzi wa filamu na uigizaji (kati ya wanafunzi wa uzamili wanaosoma kozi ya uigizaji na filamu chuo kikuu cha Dar es Salaam) ilitofautiana kulingana na ubobezi katika fani husika. Kwa

maana hiyo mtu ambaye hakuwa na maarifa ya filamu na uigizaji alionekana hafai katika utafiti huu. Powell na Connaway (2004) anasema kuwa katika uteuzi wenye madhumuni maalum sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo ambavyo vinahusiana na maswali ya utafiti kulikoni kigezo cha uteuzi nasibu au wa kubahatisha. Hivyo basi, Katika mbinu hii wahojiwa huteuliwa kwa madhumuni maalumu kutokana na nafasi zao kwa imani kuwa ndio raslimali ya data ya utafiti na mtafiti anawategemea ili kupata data toshelevu.

Sababu nyingine ambayo ilimfanya mtafiti kutumia mbinu hii ni kwamba: mtafiti alikuwa na taarifa juu ya uwepo wa makundi yenye ujuzi, maarifa na uzoefu katika uigizaji, utengenezaji na uandaaji wa filamu na fasihi ya lugha ya Kiswahili, makundi haya ndiyo raslimali ya data ya utafiti huu. Hivyo basi, mbinu hii ilitumika kuteua sampuli kutoka kwa walengwa wa utafiti huu. Kwa mfano, kwa kuzingatia kigezo hicho, waandaaji na waongozaji wa filamu waliteuliwa kwa sababu sababu inaeleweka kuwa wana ufahamu, uzoefu na maarifa katika mambo ya filamu

Vile vile mbinu hii ilitumika kuwateua waigizaji wa filamu kwa kutumia kigezo kuwa wana maarifa na uzoefu katika uigizaji na utendaji katika filamu. Walikuwa karibu na wanamfahamu Kanumba kwa karibu zaidi na hivyo ilikuwa rahisi kupata data juu ya namna ambavyo filamu zake zinamchora mwanamke katika jamii. Wanafunzi wa fasihi na wanafunzi wa uigizaji na filamu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walichaguliwa kwa kuzingatia kwamba wana uelewa na maarifa ya nadharia na mbinu za katika matumizi ya lugha katika fasihi na pia nadharia na mbinu za uigizaji na filamu. Hadhira ya filamu za Kanumba, hawa walichaguliwa kwa

kuzingatia kuwa wao ndio watazamaji na mashabiki wa filamu za Kanumba, hivyo walikuwa na uwezo wa kuelezea na kutoa maoni yao juu ya mtazao wao kuhusu ujinsia katika filamu za Kanumba.

Kwa ujumla mbinu ya madhumuni maalumu ilimsaidia mtafiti kupata sampuli ya watu wenye uzoefu, stadi na maarifa katika nadharia na mbinu za tafsiri na isimu ya lugha kwa ujumla wake na hatimaye kupata data ambazo zimekuwa ni mhimili wa utafiti huu. Vile vile data zilizopatikana kwa makundi hayo zilimsaidia mtafiti kupata na kufanya majumuisho mahususi kulingana na malengo ya utafiti. Mtafiti aliweza kupata data kutoka katika makundi hayo kutokana na sifa, maarifa, uzoefu na ujuzi walio nao katika filamu.

3.4.2 Uteuzi Nasibu

Mbinu nyingine ambayo ilitumika katika uteuzi wa sampuli ni mbinu ya uteuzi nasibu. Kombo na Tromp (2006) wanaielezea mbinu hii kuwa ni mbinu ambayo hutumia watu ambao ni hadhira tekwa, yaani watu ambao mtafiti anakutana nao bila kutarajia. Katika mbinu hii wahojiwa huwa ni wale watu ambao hutokea wakiwa wanapita au wanaonesha kupendezwa na utafiti husika. Sababu ambayo ilimfanya mtafiti kutumia mbinu hii ni kwamba: mtafiti alizingatia kuwa haikuwa rahisi kuwapata hadhira ya filamu za kanumba kirahisi. Hivyo mtafiti alitumia mbinu hii kuwateua hadhira ya filamu hasa kwa kuwaeleza watu aliokutana nao kuhusu kile anachokifanya katika utafiti wake. Wale waliopendezwa na lengo la utafiti huu walijitolea kutoa data ambazo zilihitajika katika utafiti huu. Hasa wale ambao walikuwa wamekwisha zitazama falamu za Kanumba ambazo mtafiti alizifanyia

kazi. Hii inatokana na ukweli kwamba filamu za Steven Kanumba ni nyingi na hivyo si kila mtu kaziona na kuzitazama filamu zote. Hivyo mtafiti alitumia mbinu hii kuwapata hadhira ambao wamekwisha zitazama filamu za Steven Kanumba ambazo zinafanyiwa uchunguzi katika utafiti huu.

3.5 Sampuli ya Utafiti

Sampuli ya utafiti huu ilihusisha waigizaji 10 ambao wamefanya kazi na Kanumba, hadhira 50, wanafunzi wa filamu na uigizaji 30 na wanafunzi wa fasihi 30. Ambao kwa ujumla wao waliteuliwa kutokana na uzoefu, maarifa na stadi katika mbinu na nadharia katika filamu. Washiriki hao walipatiwa dodoso lenye maswali ambayo walitakiwa kuyajibu. Sampuli ya waigizaji ilitumika katika utafiti huu ambapo waigizaji 10 walishirikishwa katika utafiti huu. Hawa kama ilivyokwisha elezwa waliteuliwa kwa kuzingatia kwamba ndiyo walengwa wa filamu kwa sababu wao ni watendaji na wana uzoefu katika kuigiza filamu na wameshirki katika kuigiza filamu za Steven Kanumba.

Hivyo basi mtafiti alitumia maswali ya usaili funge katika kuwahoji waigizaji ili kuibua uelewa wao wa maana za maneno yaliyotumika katika kumsawiri masuala ya kijinsia katika filamu za Steven Kanumba na maoni na mtazamo wao juu ya filamu hizo kuhusu masuala ya jinsia katika jamii. Maswali ya ziada pia yaliibuka kulingana na muktadha.

Upatikanaji wa waigizaji ulikuwa ni rahisi tofauti na jinsi ambavyo mtafiti alitegemea hapo awali. Walitoa ushirikiano wa kutosha na walionyesha kuupenda utafiti huu na hivyo wakawa huru kutoa data za kutosha. Sampuli nyingine ya utafiti

huu ilihusisha hadhira ya filamu ambao ni watazamaji na mashabiki wa filamu za Steven Kanumba. Hadhira ya watu 50 ilihusishwa katika utafiti huu na hivyo walishiriki katika kutoa data zinazohusiana na utafiti huu. Aidha usaili uliofanyika ni usaili funge ambapo mtafiti aliandaa maswali ya usaili na pia usaili huru ulitumika hasa pale ambapo mtafiti alitaka kupata taarifa za ziada maswali ya ziada yaliulizwa. Usaili huru pia ulifanyika ili kupata data na maelezo ya ziada kuhusiana na asili ya maneno na ishara mbalimbali zilizotumika katika filamu za Kanumba.

Sampuli ya utafiti huu ilihusisha wanafunzi wa filamu na uigizaji kutoka chuo kikuu cha Dar es salaam. Wanafunzi 30 walipatiwa dodoso ambalo lililenga kuchunguza masuala ya kijinsia katika filamu na uigizaji. Aidha wanafunzi wa fasihi 30 walihusihwa katika utafiti huu ambapo maswali ya dodoso na usaili yenye lengo la kuchunguza namna lugha inavyotumika katika kuibua mausala ya kijinsia katika jamii yalitolewa kwa wahojiwa na hivyo kupata data za kutosha katika utafiti huu. Kwa ujumla sampuli hiyo ndiyo iliyotumika katika kukusanaya data za utafiti huu. Kwa idadi hii ya wahojiwa tuliweza kupata data toshelevu na hatimaye kufanya majumuisho ya matokeo kutokana na sampuli hiyo. Kielelezo kifuatacho kinaonyesha idadi ya sampuli iliyotumika katika utafiti huu.

Kielelezo 3. 1 Washiriki wa Utafiti

NAMBA	WASHIRIKI	IDADI
1.	Waigizaji	10
2.	Wanafunzi wa kozi ya filamu na uigizaji	30
3.	Wanafunzi wa fasihi	30
4.	Hadhira	50
	Jumla ya Wahojiwa	120

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti, 2013

Kielelezo namba 3.1 kinaonyesha jumla ya sampuli yote iliyotumika katika utafiti huu. utafiti huu ulitumia jumla ya wahojiwa 120. Sampuli hiyo ilipatiwa dodoso na usaili, wakati wengine walipatiwa dodoso na wengine walifanyiwa usaili tu. Hivyo basi, kwa kufanya hivi mtafiti aliweza kukusanya data za kutosha na data zilizopatikana katika dodoso na usaili zilisaidia katika kujadili uswairi wa kijinsia katika filamu za kanumba zilizoteuliwa katika utafiti huu.

3.6 Mapendekezo

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa kijinsia katika filamu za Kanumba. Imegundulika kuwa kazi za filamu ni kazi za fasihi zenye dhima ya kuelimisha, kuburudisha, kukosoa, kutunza amali za jamii na kuadibu jamii. Kazi za filamu hubeba mielekeo ya kijamii na huwasilisha mielekeo na mitizamo ya kijamii na suala la ujinsia likiwemo. Utafiti huu ni utafiti ambao unafungua njia katika eneo la filamu. Inapendekezwa kuwa watafiti wengine wafanye tafiti zaidi kuhusu fani na maudhui katika filamu, mitindo na pia utunzi na utungaji wa filamu. Kwa kufanya hivyo tutaweza kuongeza maarifa zaidi katika taaluma ya filamu na fasihi kwa ujumla.

3.7 Utafiti Tangulizi

Matafiti alifanya utafiti tangulizi kwa kutazama na kuchambua filamu za kanumba ili kuona kama data alizozikusudia katika utafiti huu zilipatikana kwa urahisi. Lengo la utafiti huu tangulizi lilikuwa ni kujaribu kuzipima zana za utafiti na mbinu za kukusanyia data ambazo mtafiti alitegemea kuzitumia katika utafiti huu. Mtafiti alitaka kuchunguza endapo zana hizo zinafaa, zinawezekana na zinaweza kutupatia data toshelevu pindi tutakapofikia katika utafiti mkuu. Tukirejelea Baker (1994),

Kothari (2004), Kombo na Tromp (2006) na Polit, Beck na Hungler (2001) wanafasiri utafiti tangulizi kuwa ni utafiti mdogo ambao unafanyika kabla ya utafiti mkubwa. Hufanyika kwa lengo la kupima zana za utafiti kama vile dodoso au mwongozo wa usaili na pengine kupima hatua za utafiti kwa lengo la kuimarisha na kuboresha mchakato wa kukusanya data za utafiti mkuu.

Utafiti tangulizi ulifanyika kupima thamani halisi ya dodoso. Kutokana na sababu kadha wa kadha dodoso nne zilipimwa (angalia kiambatisho namba 1,2,3 na 4). Sababu ya kwanza ya kupima ufaavu wa dodoso hizo ilikuwa ni kujua kama zipo wazi na zinaeleweka kwa kile ambacho dodoso hizo zililenga kuchunguza na endapo zinaweza kutupatia matokeo stahiki. De Vaus (1993) anadai kuwa moja ya faida ya kufanya utafiti tangulizi ni kwamba unaweza kupata onyo la awali kuhusu kama utafiti mkuu unaweza kushindwa, pengine hatua fulani inaweza isiwe ina ruhusiwa au pengine zana za utafiti zilizopendekezwa zinafaa au ni ngumu.

Sababu nyingine ilikuwa ni kupima hatua za utafiti na mbinu mbalimbali za kuzitumia dodoso. Matumizi ya dodoso yalipangwa kufanywa kwa kutumia mikabala miwili. Kwanza; ni kuwaweka watu katika chumba na kuwaomba wajibu dodoso walizopewa na kisha mtafiti alizikusanya, pili; ni kuwapatia wahojiwa dodoso na kuwapa muda ambao walipaswa kuzirudisha kulingana na makubaliano baina ya mtafiti na washiriki juu ya muda muafaka wa kuzikusanya. Kutokana na utafiti tangulizi iligundulika kwamba njia ya awali ilikuwa ni bora zaidi kuliko njia ya pili hii ni kwa sababu baadhi ya washiriki hawakuweza kurudisha dodoso kwa wakati na pia ilikuwa ni usumbufu kwa mtafiti kufatilia na zipo baadhi ya dodoso

ambazo hakuzipata. Kwa upande mwingine njia ya pili ilikuwa ni bora zaidi kuwapatia washiriki ili wapate muda wa kuzisoma matini zilizotafsiriwa na waweze kutoa data zenye uhakika tofauti na kuwapa wajibu hapo hapo. Mbinu hii ilifaa kwa dodoso za wanafunzi, waigizaji na hadhira. Hata hivyo, kwa upande wa mbinu ya kwanza ilitumika zaidi kwa waongozaji wa watalii na wahifadhi mila. Kwa maana hiyo kutokana na utafiti tangulizi tulijifunza kwamba ilikuwa bora kutumia mbinu zote katika kugawa na kutumia dodoso kama zana ya kukusanyia data. Kwa mfano haikuwa rahisi kuwakusanya wataalamu wa tafsiri wote kwa pamoja katika chumba na kuwagawia dodoso. Hivyo kwa upande huu ililazimika kuwapatia dodoso na kupanga muda wa kuzikusanya.

Dodoso kwa ajili ya wanafunzi wanaosoma kozi ya fasihi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ziligawiwa kwa wanafunzi kumi ambao walikuwa wanasoma uzamili katika tafsiri. Dodoso zilitumiwa kwa kutumia njia mbili kwanza kundi la watu watano waliwekwa pamoja katika chumba na kisha kupatiwa dodoso ili wajibu maswali ya dodoso na kisha mtafiti alizikusanya. Kwa upande mwingine kundi lingine la watu watano walipatiwa dodoso na kisha mtafiti alikubaliana nao siku ya kuzirudisha dodoso hizo. Lakini njia hii ilikuwa na changamoto kubwa kwa sababu baadhi ya dodoso hazikuweza kurudi na hata zilizorudi zilipatikana kwa shida na wakati mwingine mtafiti alikuta hazijajazwa kwa madai kwamba wahojiwa hawana nafasi ya kutosha.

Hivyo basi mbinu hii ilihitaji ufuatiliaji wa karibu na wa mara kwa mara. Hivyo basi, kutokana na uzoefu huu alioupata mtafiti aligundua kuwa mbinu hii ya namna ya

kuzitumia dodoso ni ngumu sana na inahitaji uvumilivu mkubwa. Vinginevyo, kwa funzo hilo ni vema kutumia njia ya awali ambapo mtafiti anagawa dodoso na wahojiwa wanajibu kwa wakati huo na kisha anazikusanya.

Aidha, mtafiti pia alipima kuhusu ubora wa maswali yaliyoulizwa katika dodoso kama yapo wazi na yanajibika kirahisi na kueleweka kwa washiriki. Mtafiti aligundua kuwa yapo maswali ambayo yalikuwa hayawezi kujibika, mengine yalikuwa na utata na mengine yalikuwa hayawezi kutufikisha kwenye lengo la utafiti huu. Hivyo basi maswali yote yaliyoonekana yana matatizo yalifanyiwa marekebisho kabla ya kuanza ukusanyaji wa utafiti mkuu.

Kwa ujumla utafiti tangulizi uliweza kumsaidia mtafiti kujua yafuatayo;

i) Kuwapatia wahojiwa maswali ya dodoso kama ambavyo angefanya katika utafiti mkuu
ii) Kurekodi muda uliotumika kujaza dodoso (muda ulionekana kuwa ni muda muafaka)
iii) Kutumia matokeo ya dodoso kuona ubora na ufaavu wa maswali yaliyoulizwa
iv) Kufanya marekebsho kwa maswali magumu na yenye utata, kuondoa maswali ambayo hayana mchango mkubwa katika utafiti na pia kutoa fasili ya maneno magumu
v) Kuzitunza data zilizopatikana ili ziweze kutumika katika uchambuzi wa data za utafiti mkuu.

Kwa upande mwingine maswali ya dodoso yalitolewa kwa waongozaji wa filamu, wasanii na hadhira. Njia iliyotumika ni kuwaweka pamoja wahojiwa wote katika

makundi yao katika chumba kisha kuwapa dodoso wajaze na baada ya muda mtafiti alizikusanya dodoso. Katika dodoso hizo kuna baadhi ya maswali yalikuwa magumu, hayaeleweki, yana utata na mengine yalionekana kutokuwa na mchango katika utafiti huu. Mtafiti aligundua hayo baada ya wahojiwa kuuliza maswali kama vile; ’swali hili lina maana gani?’ kama ilivyokwisha elezwa maswali haya yaliondolewa katika utafiti mkuu.

Hii ilimsaidia kuona endapo maswali yanajibika na yana mchango wowote katika utafiti huu. Kwa kufanya hivi mtafiti aliweza pia kufanya marekebisho ya maswali ya mwongozo wa usaili ili kuwa na maswali yenye manufaa kwa utafiti huu. Katika kufanya usaili kuna changamoto ambazo mtafiti alikumbana nazo; mtafiti alikuwa hajapata pesa ya kukusanyia data hivyo hakuwa na vifaa kama vile tepu rekoda, video kamera na kamera ya kawaida. Hivyo basi, wakati wa usaili mtafiti alitegemea kuandika kila kitu kwenye notibuku. Kwa ujumla mtafiti aliona kuwa zoezi hili lilikuwa kwa ajili ya kupima kuona kama mbinu hii ya usaili inafaa na je maswali yanayoongoza katika usaili yana ubora na ufaavu kiasi gani?

Kwa maana hiyo mtafiti alirudia kufanya usaili na watu hawa wakati wa utafiti mkuu ili kupata data ambazo pengine hakuzipata, kupata taarifa za ziada na ufafanuzi wa mambo ambayo yalipatikana na hayakueleweka katika utafiti tangulizi. Kwa kufanya hivi mtafiti aliweza kugundua ufaavu wa mbinu hii ambapo aliweza kugundua kuwa inaweza kutufikisha kwenye malengo ya utafiti huu.Mtafiti hakuweza kufanya utafiti mdogo katika maeneo mengi kwa sababu kipindi utafiti mdogo unafanyika mtafiti hakuwa na pesa za kukusanyia data.

Mwisho kabisa, inapaswa ieleweke kwamba data zote zilizopatikana katika utafiti tangulizi zilihusishwa katika uchambuzi wa data za utafiti mkuu, ambao ndiyo utafiti huu. Kama anavyoeleza Holloway (1997) kuwa katika ukusanyaji wa data watafiti wanashauriwa kutumia baadhi au data zao zote walizokusanya kwenye utafiti tangulizi kwa sababu ukusanyaji na uchambuzi wa data katika utafiti uso wa kitakwimu ni mwendelezo. Holloway alitolea mfano wa mwendelezo wa usaili katika usaili huru, ambapo usaili wa pili unatokea kuwa bora kuliko usaili uliotangulia kwa sababu usaili umepata mwanga kutoka katika usaili uliotangulia ambao umetumika kuboresha ratiba ya usaili na maswali mahsusi. Kwa hiyo si muhimu kutenganisha data zilizokusanywa kutokana na tafiti hizi mbili mtu anapofanya utafiti usio wa kitakwimu. Ikumbukwe kuwa utafiti huu unatumia nduni na sifa za tafiti za kitakwimu na zisizo za kitakwimu.

3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji data ni shughuli ya kukusanya data katika uwandani kwa kuwahoji wasailiwa (rejea Kothari, 2004). Zipo mbinu mbalimbali za ukusanyaji data wa kila mbinu ina ubora wake na inafaa kukusanya data za utafiti. Lakini ufaavu wa mbinu za ukusanyaji data hutegemea na malengo ya utafiti, muda na tatizo la utafiti. Hivyo basi, kutokana na malengo ya utafiti huu, mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ni nne ambazo kwa ujumla wake zinakamilishana na kujazilizana, nazo ni:

i) Mbinu ya maktaba

ii) Mbinu ya usaili

iii) Mbinu ya dodoso

iv) Mbinu ya majadiliano ya vikundi

Zipo sababu mbalimbali ambazo humfanya mtafiti kuamua kutumia mbinu zaidi ya moja katika kukusanya data. Kwa mujibu wa Kothari (2004) anasema mtafiti huamua kutumia mbinu za utafiti zaidi ya moja. Hivyo basi, katika utafiti huu sababu iliyopelekea kutumia mbinu za ukusanyaji data zaidi ya moja ni kwamba: zitatusaidia kupata data ambazo zisingelipatikana kwa njia moja peke yake. Kama anavyosema Alderson (1992) hakuna mbinu iliyo bora katika utafiti ikitumika peke yake. Ni vema kukusanya data kutoka katika vyanzo na mbinu mbalimbali ili mtafiti aweze kuhakiki matokeo kupitia mbinu hizo.

Katika utafiti huu mbinu hizo zilitumika kwa kukamilishana na kujazilizana, mbinu ya uchambuzi maudhui iliambatana na usomaji na uchambuzi wa matini za filamu za Kanumba ambazo ziliteuliwa kwa kipindi chote cha utafiti. Zoezi hili lilifanyika ili kupata data zinazohusiana na usawiri wa jinsia katika filamu za Kanumba. Wakati mbinu ya usaili na dodoso zilifanyika ili kuchunguza ni jinsi gani ujinsia unajitokeza katika filamu hizo kwa kutumia vipengele vya lugha. Mbinu za ukusanyaji data na utumiaji wake zinajadiliwa katika sehemu ndogo zifuatazo hapa chini.

3.7.1 Mbinu ya Maktaba

Kothari (2004) anaielezea mbinu hii kuwa ni mbinu inayohusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo. Sababu ya kuchagua kutumia mbinu hii ni kwamba inafahamika kuwa tafsiri huwa katika matini mbili

zilizoandikwa (rej. Cartford, 1965; Newmark, 1981 na Mwansoko 1996). Nao Pyne & Weber (2007) wanasema kuwa matini hutoa taarifa za awali. Kwa maana hiyo, matini andishi ndiyo chanzo kikuu cha data ya tafsiri. Katika utafiti huu matini andishi ndiyo ilikuwa chanzo kikuu cha data ya utafiti huu. Ilionekana kwamba ili tuweze kupata data ni lazima tuchambue na kulinganisha maudhui ya matini za filamu za Steven kanumba. Hivyo basi, kwa kutumia mbinu hii tuliweza kuchambua, kulinganisha na kubainisha maneno na maana katika matini za filamu za Kanumba.

Kwa kutumia matini hizi mtafiti alibainisha na kuchambua maneno yenye maudhui yanayosawiri masuala ya kijinsia katika jamii. Baada ya zoezi hilo, mtafiti aliyaorodhesha maneno hayo na kisha kuyatumia katika dodoso ambapo wahojiwa waliombwa kutoa maana ya maneno hayo katika muktadha wa kijamii.

3.7.2. Mbinu ya Usaili

Babbie (1992) anasema kuwa usaili unahusisha mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na wahojiwa na mtafiti hupata maelezo zaidi kuhusu baadhi ya mambo ambayo yasingeweza kuwekwa bayana kupitia mbinu nyingine ya utafiti. Sababu ya kuchagua kutumia mbinu hii ni kwamba ni mbinu inayoruhusu unyumbukaji katika mchakato wa kuuliza maswali, kuweka bayana istilahi ambazo zinaonekana hazieleweki kwa watu na kupata taarifa za ziada na za kina zaidi, hususan pale ambapo majibu ya watu wanaosailiwa hayaeleweki (rej. Kothari, 1990 na 2004). Hivyo basi, mbinu hii ilifaa sana na kutusaidia kukusanya data za kutosha na zilizo yakini zaidi. Katika utafiti huu, usaili wa aina mbili ulitumika yaani, *usaili funge* na *usaili huru*.

Usaili funge ni usaili ambao seti ya maswali huandaliwa katika mpangilio na maswali huulizwa hatua kwa hatua kufuatana na mpangilio huo (Kothari, 2004). Kwa kutumia usaili funge, mtafiti aliandaa maswali ambayo yalikuwa ni maswali ya mwongozo wakati wa kufanya usaili. Maswali haya yaliulizwa hatua kwa hatua kulingana na kundi la wahojiwa. Kila kundi lilikuwa na maswali yake ambayo yalikuwa yameandaliwa katika mpangilio kulingana na malengo ya utafiti huu. Hivyo basi, wahojiwa wote waliuizwa maswali sawa kulingana na maswali ya mwongozo wa usaili yaliyoandaliwa. Usaili ulifanyika kwa waigizaji wa filamu, hadhira, wanafunzi wa fasihi na wanafunzi wa filamu na uigizaji. Wakati wa usaili mtafiti alitumia tepu rekoda kurekodi mazungumzo baina yake na wahojiwa, vile vile alitumia shajara kuandika majibu yaliyotolewa na wahojiwa na pia alitumia video kamera na kamera ya kawaida kupiga picha na kuchukua kumbukumbu za utafiti huu. Data zilizohifadhiwa katika zana hizo zilimsaidia mtafiti katika uchambuzi wa data, kwa mfano mtafiti aliweza kusikiliza tepu rekoda pale ambapo yale aliyoyaandika kwenye notibuku hayaeleweki au kuna vitu ambavyo ameviruka katika kurekodi katika shajara. Hivyo basi, kwa kutumia mbinu hii, mtafiti aliweza kupata data ambazo zilimsaidia kufanya majumuisho ya data za utafiti huu.

Kwa upande mwingine, usaili huru ni usaili ulio huru katika uulizaji wa maswali na haufuati mfumo wala mbinu maalumu ya kuhifadhi taarifa. Hivyo katika utafiti huu maswali kwa ajili ya usaili yaliandaliwa na pia maswali mengine yaliibuka kulingana na muktadha. Mtafiti alitumia usaili ulio wazi kuuliza maswali ya ziada hasa alipotaka kupata ufafanuzi juu ya jambo ambalo aliliona halijaeleweka ama aliliona lina mchango kubwa katika utafiti huu.

3.7.3 Mbinu ya Dodoso

Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu hii huhusisha uandaaji wa dodoso ambalo hutumwa kwa mhusika na ombi la kumtaka kujibu maswali yaliyomo katika dodoso hilo na hatimaye kurudisha kwa mtafiti. Dodoso huhusisha orodha ya maswali ambayo huwekwa katika mpangilio na utaratibu maalumu. Kothari (1990) anasema kuwa katika kiwango cha mahojiano ya msingi ya utafiti uso wa kitakwimu, undani na taarifa za ziada kuhusu hisia, uzoefu na maarifa ya wahojiwa hujionyesha vema kupitia maswali funge. Hivyo basi, katika utafiti huu mtafiti aliandaa maswali mengi kadri iwezekenavyo ili kuwapa uhuru na nafasi wahojiwa kujibu kwa uhuru na kuelezea hisia, uzoefu na maarifa waliyonayo juu ya mada huisika. Powell na Connaway (2004) wanatoa sababu ya kupata data kwa njia ya maswali yaliyo wazi kuwa humwezesha mtu kuelewa na kung'amua mtazamo wa watu bila kushawishi mtazamo huo kabla hawajaonesha uelewa wao kuhusu suala hilo. Akishadidia mawazo hayo, Patton (2002) anaeleza kuwa ili kuteka umaizi ama utambuzi wa washiriki unapaswa kuwapa nafasi kubwa ya kuelezea hisia zao, mawazo, uchunguzi na uzoefu wao. Kwa hiyo, kazi ya mtafiti hapa ni kutoa mwongozo ambao kwao, watu wanaweza kujibu katika njia amabyo inawasilisha uwazi na mtazamo wao kuhusu ulimwengu unaochunguzwa, mawazo yao kuhusu kile kinachoendelea, uzoefu wao na msingi wa utambuzi wao.

Hivyo basi, sababu ya kuamua kutumia mbinu hii ni kwamba inaeleweka kuwa kwa kutumia dodoso, mhojiwa huwa huru kuelezea hisia, mawazo na maoni yake juu ya jambo fulani kwa uwazi zaidi. Hivyo basi, mbinu hii ilitusaidia kupata data za kutosha na kwa uwazi zaidi kwa kuwapa wahojiwa nafasi ya kuelezea mawazo,

hisia, mtazamo na uzoefu wao (rej. Patton, 2002). Katika utafiti huu, maswali ya dodoso (taz. Kiamabatisho 1, 2 na 3) yaliandaliwa ili kukidhi mahitaji ya malengo ya utafiti huu (rej. Kipengele namba 6.2.2).

Katika mchakato wa kukusanya data, Wanafunzi wa kozi ya fasihi, waigizaji, wanafunzi wa filamu na uigizaji na hadhira walipewa dodoso. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliweza kupata data ambazo zilisaidia kufikia kwenye malengo ya utafiti huu. Katika dodoso zote mtafiti alitunga maswali mengi yaliyo wazi ili kuweza kukusanya taarifa zaidi juu ya namna ambavyo filamu za Kanumba zinaswairi masuala ya kijinsia katika jamii.

3.7.4 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi

Mbinu hii ilitumika katika kufanya majadiliano ya vikundi ambapo mtafiti aliwahusisha hadhira katika makundi na kufanya nao majadiliano juu ya filamu za Kanumba na usawiri wa ujinsia katika filamu zake. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliweza kuibua masuala mbalimbali ya kijinsia na namna yanavyojitokeza katika fialmau za Kanumba. Hivyo basi mbinu hii ilikuwa bora kwa sababu ilimsaidia mtafiti kupata data za kutosha kuhusiana na masuala ya kijinsia katika filamu za Kanumba.

Kwa kutumia mbinu hii mtafiti alitumia tepu rekoda kurekodi mazungumzo na mijadala iliyofanyika katika chumba cha majadiliano. Hii ilimsaidia baada ya mjadala kuweza kufanya uchambuzi wa data alizozipata. Mtafiti aliweza kuibua hisia, mtazamo na mielekeo ya hahdiara kuhusu ujinsia katika filamu za Kanumba na hatimaye kufanya majumuisho ya utafiti huu.

3.8 Zana za Kukusanyia Data

Katika utafiti huu zana za kukusanyia data zimegawanyika katika makundi sita. Makundi hayo ni kama ifuatavyo:

3.8.1 Matini

Matini tunazozizungumzia hapa ni matini za filamu za Kanumba ambazo mtafiti alizikusanya ili kupata data anazokusudia.

3.8.2 Ngamizi na Shajara

Hapa tunapozungumzia kompyut,a tunarejelea kompyuta ya mkononi yenye programu ya kinasa sauti na notibuku za kuandikia kumbukumbu. Zana hizi ni muhimu sana katika kukusanyia na kuhifadhi data za awali kipindi cha mazungumzo. Katika utafiti huu zilitumika kukusanya na kurekodi data zilizokusanywa katika dodoso na usaili.

3.8.3 Kinasa Sauti

Vinasa sauti vitatumika kurekodi sauti wakati wa mazungumzo baina ya mtafiti, hadhira na wasanii. Kwa kufanya hivi mtafiti aliweza kupata data zinazohusiana na mwelekeo wa jamii kuhusu suala la jinsia katika filamu za Kanumba.

3.8.4 Video kamera na Kamera ya Kawaida

Video kamera ilitumika kurekodi na kuchukua matukio katika muktadha na mazingira ya utafiti. Vile vile, kipindi cha mahojiano baina ya mtafiti na wasanii na hadhira. Pia kamera ya kawaida ilitumika kuchukua picha mbalimbali wakati wa utafiti mtafiti anapokuwa uwandani na matukio mbalimbali katika eneo la utafiti.

3.8.5 Dodoso

Dodoso tatu za maandishi ziliandaliwa kwa ajili ya wahojiwa. Dodoso ya kwanza ililenga kuchunguza uelewa wa maana za maneno kwa hadhira. Hapa mtafiti aliorodhesha baadhi ya maneno yanayotumika katika filamu za Kanumba na kuwapatia wahojiwa ili watoe maana ya dhana hizo. Dodoso la pili lililenga kuchunguza ujinsia na jinsi usawiri wake katika filamu za Kanumba na hojaji ya tatu italenga kuchunguza maana na mwelekeo wa jamii kuhusu suala la jinsia na jinsi linavyojitokeza katika filamu za Kanumba. Hojaji hizi zilitolewa kwa hadhira na wasanii.

3.8.6 Usaili

Kama ilivyokwisha elezwa hapo awali, maswali kwa ajili ya usaili yaliandaliwa kwa ajili ya wasanii na hadhira. Hapa kulikuwa na maswali ya usaili ambayo si rasmi ambayo mtafiti aliyaandaa kabla ya kwenda uwandani na maswali hayo yaliulizwa kwa kila mhojiwa. Aidha, mtafiti aliuliza maswali ya ziada ambayo yaliyoibuka kulingana na muktadha.

3.9 Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu mbili, yaani *uchambuzi maudhui* na *uchambuzi linganishi*. Mbinu ya uchambuzi maudhui inaelezewa na Kombo na Tromp (2006) kuwa ni mbinu ya uchambuzi ambayo huziweka mada kulingana na jinsi zinavyofanana na kuhusiana. Sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba ilisaidia kuweka maana zote zinazohusiana kutokana na data za dodoso na usaili ili kutoa mawazo ya jumla kulingana na malengo ya utafiti huu.

Kwa upande mwingine, uchambuzi linganishi hutumika kulinganisha data kutoka kwa watu tofauti. Mbinu hii iliteuliwa kutumika katika kuchambua data za utafiti huu kwa sababu ya uhalisia wa utafiti huu ambao unchunguza suala la ujinsia hivyo mbinu hii ilitumika kulinganisha jinsi mwanamke na mwaume wanavyosaiwiriwa katika filamu za kanumba.

Aidha, kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliweza kulinganisha mawazo, mtazamo, maoni na hisia za wahojiwa ambazo zilitolewa katika dodoso na usaili ili kupata majumuisho ya malengo ya utafiti huu. Vile vile mtafiti aliweza kulinganisha na mambo aiyoyabaini wakati akifanya majadiliano ya vikundi na uchambuzi maudhui. Katika kulinganisha matokeo aliyoyapata katika mbinu zote za utafiti alizozitumia mtafiti aliweza kutoa majumuisho ya utafiti wake kulingana na malengo mahsusi ya utafiti huu.

3.10 Hitimisho

Kwa kuhitimisha, sura hii imejadili kwa kina vipengele mbalimbali vya kimethodolojia ambavyo vimetumika katika utafiti huu ili kutoa matokeo jumuishi na hitimisho la utafiti huu. Kama ambavyo imekwishaelezwa tangu awali, mjadala wa methodolojia ya utafiti umejikita katika mkabala usio wa kitakwimu na ule wa kitakwimu. Mkabala wa usio wa kitakwimu umelenga katika kapata ufahamu wa kwa nini washiriki wanahisia, wanatenda, au wanakuwa na tabia kama walizonazo katika muktadha fulani. Utafiti usio wa kitakwimu ulisaidia sana kupata taarifa zaidi kutoka kwenye uelewa wa watu, hisia na uzoefu wao mambo ambayo yasingeweza kupatikana kwa kutumia mbinu nyingine za utafiti (Silverman, 2000 na 2005). Vile

vile katika mchakato wa kukusanya data, mkabala usio wa kitakwimu huruhusu matumizi ya mbinu za kukusanyia data zaidi ya moja. Hii ilimsaidia mtafiti kuchunguza na kuthibiti uthabiti wa data. Kwa kutumia uteuzi wa sampuli wenye madhumuni maalumu, ulimsaidia mtafiti kupata sampuli ambayo iliweza kutoa taarifa zilizohusiana na utafiti huu. Mbinu za utafiti zisizo za kitakwimu ambazo zilitumika kukusanya data zilitumika kumwezesha mhojiwa kuelezea uzoefu wao kwa kutumia lugha na maneno yao binafsi. Zaidi ya hapo mkabala huu husisitiza matumizi ya data za mdomo kutoka uwandani kwa kuzinukuu au kwa kuziweka katika makundi madogo madogo ambayo yanamsaidia mtu kupata taswira halisi ya kile kinachoendelea katika jamii iliyofanyiwa utafiti. Haya ni mambo ya msingi katika uchambuzi wa data na kutoa utetezi wa matokeo ya data za utafiti huu. Mtafiti aliweza kuchambua data na kwa kutoa baadhi ya nukuu za maneno ambayo yalisemwa au kuandikwa na wahojiwa bila kuyapunguza au kuyaongeza kwa kutumia takwimu au ufalaguzi.

Vile vile utafiti huu ulitumia mkabala wa utafiti wa kitakwimu ambao ulisaidiana na utafiti wa usio wa kitakwimu kukusanya data na kuchambua data za utafiti huu. Hivyo basi, matumizi ya mikabala yote miwili ilisaidia kupunguza mapungufu ya mkabala mmoja na mkabala mwingine. Sura inayofuata inachambua na kujadili data zilizokusanywa ili kukidhi malengo mahsusi ya utafiti huu.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa kijinsia katika filamu za Steven Kanumba ili kuona ni jinsi gani filamu hizo zinasawiri na kuibua masuala ya kijinsia katika jamii. Kwa ujumla sura hii inajaribu kujibu maswali manne ya msingi ambayo yaliibuliwa katika sura ya kwanza kwa kuzingatia muktadha wa filamu za Steven Kanumba. Sura hii ina sehemu kuu nne sehemu ya kwanza inahusu muhtasari wa Filamu teule, sehemu ya pili ni vipengele vya lugha vilivyotumika katika fialamu za Steven Kanumba, sehemu ya tatu inahusu mdafao wa ujitokezaji wa vipengele vya lugha katika filamu za Steven Kanumba, sehemu ya nne inahusu usawiri wa ujinsi katika filamu za kanumba, sehemu ya tano inahusu nafasi ya mwanamke katika filamu za kanumba, sehemu ya sita ni tofauti ya mwanamke na mwanaume katika filamu za Steven Kanumba na sehemu ya saba ni hitimisho.

4.2 Muhtasari wa Filamu Zilizofanyiwa Uchunguzi

Kama ilivyokwisha elezwa tangu awali filamu zilizofanyiwa uchunguzi ni filamu ya Moses, My Valentine na Johari. Katika filamu hizo utafiti huu ulichunguza vipengele vya lugha na jinsi vinavyotumika kusawiri suala la ujinsia katika jamii. Sehemu ifuatayo inatoa muhtasari wa filamu hizo kwa ufupi.

4.2.1 Moses

Filamu hii inahusu masuala ya kijinsia kwa kubainisha nafasi ya mwanamke katika jamii. Inaonyesha namna mwanamke anavyoweza kuathiri maisha ya watoto wake na

kuwajengea chuki isiyoisha. Inaonyesha uwezo wa mwanamme na mapungufu ya mwanamke katika maamuzi ndani ya jamii. Inaonyesha mahusiano ya mwanamke na mwanamme katika suala la mapenzi, mahusiano ya mama na mtoto katika jamii.

4.2.2 My Valentine

Filamu hii inahusu suala la ndoa na mapenzi. Inaelezea juu ya matatizo ya uzazi ambayo jamii inamsukumia lawama mwanamke. Filamu hii inajaribu kutoa suluhisho la kupata mtoto ama kukosa linamhsusu mke na mume na si mke pekee.

4.2. 3 Johari

Johari ni filamu inayohusu suala la UKIMWI. Filamu hii inaibua juu ya namna ugonjwa wa UKIMWI unavyooenezwa na athari zake kwa jamii. Aidha filamu hii inatoa suluhisho la maisha ya waathirika wa UKIMWI na kwamba UKIMWI siyo kifo na mtu mwenye ugonjwa huu anaweza kuoa ama kuolewa na kuishi maisha yenye furaha. Filamu hii pia inaonyesha nafasi ya dini katika kutatua suala la UKIMWI.

4.2.4 She is My Sister

Filamu hii inahusu usaliti wa mapenzi amabao unafanywa na mwanaume na marafiki pia. Katika filamu hii msanii anaonyesha jinsi mwanamke alivyoweza kumnusuru mwanaume kutoka katika maisha ya umaskini hadi kufika kwenye utajiri lakini badala yake mwanaume anasariti na kumtelekeza yeye na mtoto, anamuibia kila kitu hadi vyeti vya shule na kumuacha akiwa hana kitu mkononi. Mwanaume anakimbia na mali zote na kuishi na rafiki ya mkewe. Mwisho msanii anaonyesha jinsi mwanamke alivyoweza kulipa kisasi na kukomboa mali za dada yake.

4.3 Kubainisha Vipengele vya Lugha Katika Filamu za Kanumba

Moja ya malengo mahsusi ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba. Vipengele hivi vilibainishwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui ambapo mada zinazohusiana ziliwekwa pamoja. Maneno ama sentensi ambazo zilikuwa na sifa inayofanana zilibainishwa kama aina ya kipengele cha lugha kulingana na muundo, sifa, uamilifu na dhima zilizokuwa na ulinganishaji wa kutumia viunganishi kama, mithili ya zilibainishwa kama tashibiha na maneno yaliyolinganishwa bila viunganishi kwa kutumia dhana zisizohusiana yalibainishwa kama sitiari na kadhalika. Katika utafiti huu, mtafiti alisikiliza na kutazama tamthilia alizoteua kasha kuchambua vipengele vya lugha katika filamu hizo. Utafiti huu uligundua kuwa filamu za Kanumba zilizoteuliwa hutumia lugha kama vile: kejeli na dhihaka, tashibiha, sitiari, taswira, tashihisi, ishara, misemo na methali.

4.4 Mdafao na Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha

Katika utafiti huu lengo mojawapo lilikuwa ni kuchunguza mdafao wa vipengele vya lugha vilivyobainishwa. Ili kuona ni kipengele kipi cha lugha kinachojitokeza mara nyingi zaidi katika tamthiliya za Kanumba na sababu ya uteuzi wa kipengele hicho. Katika kufanya hivi, utafiti huu ulipima kipengele gani kinachojitokeza zaidi na kimejitokeza mara ngapi katika kila filamu ambayo ilifanyiwa utafiti. Kwa kufanya hivi utafiti huu uliweza kubaini kipengele chenye mdafao mkubwa ambacho kinajitokeza zaidi na pia kuelezwa kuwa ndiyo lugha inayomtambulisha msanii huyo. Kielelezo kifuatacho kinabainisha vipengele vya lugha na mdafao wake katika filamu za Kanumba.

Kielelezo 4.1 Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha

Namba	Kipengele cha Lugha	Mdafao Katka Kila Filamu				Jumla ya mdafao
		She is my Sister	Moses	Johari	My Valentine	
1.	Sitiari	10	8	20	6	39
2.	Tashibiha	11	10	20	25	66
3.	Methali	5	4	5	3	17
4.	Tashititi	6	5	8	7	26
5.	Ishara	10	15	20	19	64
6.	Taswira	10	20	30	10	70
7.	Kejeli na dhihaka	30	20	10	20	80

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti, 2013

Ukichunguza kielelezo hicho utaona kuwa kejeli na dhihaka (80) ni kipengele cha lugha ambacho kinajitokeza zaidi katika filamu za Kanumba. Ikifuatiwa na taswira (70), tashibiha (66), ishara (64), sitiari (39), tashititi (26) na methali (17). Hivyo basi tunaweza kusema kuwa msanii huyu katika filamu zake ametumia kwa wingi kejeli na dhihaka katika kumchora kusawiri suala la ujinsia katika jamii. Matokeo haya yanaweza kuelezwa kwa muhtasari kwa kutumia chati ifuatayo.



Chati 4.1 Mdafao wa Vipengele vya Lugha Katika Filamu za Kanumba

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti, 2013

Kutokana na chati hiyo tunaweza kusema msanii Kanumba ametumia lugha ya kejeli na dhihaka kwa kiasi kikubwa zaidi kuliko vipengele vingine vya lugha. Vipengele hivi vimeonekana vimetumika katika kusawiri masuala ya kijinsia na kumchora mwanamke kulingana na nafasi yake katika jamii. Mwandishi anasawiri mtazamo na mielekeo ya jamii kuhusu mwanamke. Matokeo haya yanathibitisha kuwa, mwandishi wa kazi za fasihi huwa haendi nje ya jamii yake hivyo basi kazi za fasihi husawiri na kuwasilisha mtizamo na mielekeo ya jamii kuhusu masuala yaliyopo ndani ya jamii (Senkoro, 1982; Wamitila, 2003; Wamitila, 2010).

Hivyo basi, kutokana na matokeo ya wahojiwa katika usaili, dodoso na majadiliano ya vikundi iligundulika kuwa kejeli na dhihaka hutumiwa kujenga tamathali zingine za semi na hivyo msanii ameitumia kama mbinu ya kisanii katika kuwasilisha ujumbe wake. Kejeli na dhihaka humfanya hadhira kutafakari juu ya kile kinachozungumzwa, humpa nafasi hadhira ya kushiriki katika kazi ya sanaa kwa vitendo mfano kucheka, kukasirika, kutikisa kichwa na hata kupiga makofi. Hivyo basi, matumizi ya kejeli na dhihaka huibua hisia na mtazamo wa hadhira kuhusu kazi ya sanaa. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa lugha inayomtambulisha Kanumba ni matumizi ya dhihaka na kejeli. Tunaweza kumtofautisha Kanumba na Kezilahabi ambaye hutumia lugha ya ucheshi wakati Shaban Robert anatumia lugha ya tashititi katika kazi zake (Wamitila, 2003; Senkoro, 2012).

4.4.1 Sababu za Kutumia Kejeli na Dhihaka

Wahojiwa walipoulizwa juu ya sababu ya kujitokeza zaidi kwa kejeli na dhihaka. Walieleza kuwa matumizi ya dhihaka humsaidia mtu kuibua mambo mazito na

kuyawasilisha katika jamiii bila hofu wala wasiwasi. Ilielezwa na mmoja wa wahojiwa kuwa:

“Unajua mtu anapotumia dhihaka au kejeli inakuwa kama ni utani lakini kumbe ndiyo anakwambia ukweli wenyewe”

Matokeo yanaonyesha kwamba, katika filamu za Kanumba zilizofanyiwa uchunguzi kejeli na dhihaka ndiyo lugha ambayo imetumika zaidi katika kusawiri suala la ujinsia. Kwa mfano wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walitaja matumizi mengine ya vipengele vya lugha kama vile tashibiha, sitiari, ishara kwa pamoja vinatumika kujenga kejeli na dhihaka. Hivyo basi kwa matokeo hayo tunaona kuwa katika filamu zilizotungwa na Kanumba kejeli na dhihaka ndiyo lugha ambayo imetumika zaidi kama mbinu ya kisanii kwa lengo la kufikisha ujumbe katika jamii husika. Aidha wakati wa usaili mtafiti aliwahoji wahojiwa ambao ni wasanii, hadhira na wanafunzi wa fasihi na wanafunzi wa filamu na uigizaji sababu ya uteuzi wa vipengele hivyo vya lugha na matokeo yalikuwa; Asilimia 90% ya wahojiwa walibainisha kuwa sababu ya uteuzi wa vipengele hivyo ilikuwa ni kujenga maudhui kwa njia ya uficho ili kukosoa, kuelimisha, kuonya na kuburudisha jamii. Mbinu hii ya matumizi ya lugha ya uficho na mafumbo katika filamu ni mbinu ambayo inatumiwa na wasanii wa kazi zingine za fasihi kama vile riwaya, ushairi na tamthiliya (Senkoro, 1982).

4.5 Usawiri wa Ujinsia katika Filamu za Kanumba

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha usawiri wa ujinsia katika filamu za kanumba. Utafiti huu ulilenga kuchunguza ni namna gani suala la ujinsia linasawiriwa katika filamu za kanumba. Ili kufikia lengo hilo, utafiti huu ulijiuliza

maswali yafutayo ambayo yalikuwa kama mwongozo wa uchunguzi huu

i) Je mwanamke anachorwa vipi katika sanaa ya filamu kupitia filamu za kanumba?

ii) Je kuna tofauti baina ya mwanamke na mwanaume katika filamu hizo?

iii) Na kama kuna tofauti je ni kwa nini tofauti hizo?

iv) Na je, wasanii kama Kanumba ambao wameanza sanaa zao katika kipindi ambacho mwanamke anajaribu kujikomboa

v) Je wamebadili mwelekeo wa jamii au bado wanamtazama mwanamke kwa jicho hasi na mwanaume kwa jicho chanya?

Haya ndiyo maswali ya msingi ambayo yamejenga utafiti huu. Katika kufikia lengo hilo, mtafiti alitazama filamu za Kanumba alizoziteua na kisha kuchunguza namna ujinsia unavojitokeza kwa kupitia lugha inayotumika katika filamu hizo. Aidha mtafiti alitumia maswali ambayo aliyaandaa kama maswali ya mwongozo wakati wa majadiliano ya vikundi na hadhira ya filamu za Kanumba. Wakati wa majadiliano ya vikundi kulikuwa na muda ambao mtafiti aliweka video za filamu za Kanumba ili wahojiwa waeze kuona na kutoa mawazo yao kuhusu masuala ya ujinsia. Maswali yafuatayo yaliulizwa wakati wa usaili: Je filamu za Kanumba zinamchora mwanamke katika mtazamo hasi? Je kuna mabadiliko yoyote kuhusu nafasi ya mwanamke katika filamu za Kanumba?. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama ifuatavyo;

4.5.1 Je Filamu za Kanumba Zinamchora Mwanamke Katika Mtazamo Hasi?

Katika swali hili wahojiwa walitakiwa kujibu ndiyo au hapana. Matokeo ya dodoso yalikuwa kama ifuatavyo;



Chati 4.2 Matokeo ya Dodoso

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti, 2013

Kielelezo hicho kinaonyesha kuwa katika kujibu swali linalouliza endapo filamu za Kanumba zinamchora mwanamke katika mtazamo hasi, wahojiwa 80 walisema NDIYO na wahojiwa 30 walisema HAPANA wakati wahojiwa 10 walisema hawajui. Kwa matokeo hayo, tunaweza kusema kuwa filamu za Kanumba zinamchora mwanamke katika mtazamo hasi. Hata hivyo hatuwezi kusema kuwa Kanumba alikuwa ni mkandamizaji wa mwanamke bali tunaweza kujumuisha kuwa alikuwa ni msanii ambaye alitumia sanaa na mbinu za kisanii katika kuibua mielekeo na mitazamo ya jamii kuhusu mwanamke. Matokeo haya hayana tofauti na tafiti zingine zilizofanyika kuhusu nafasi ya mwanamke katika kazi za fasihi (Mutembei, 2001; Momanyi, 2003; Jilala, 2010/2011). Hivyo tunaweza kusema kwamba filamu kama kazi ya sanaa haitofautiani na kazi zingine za tanzu za fasihi kama vile ushairi, riwaya na tamthiliya.

Matokeo ya swali hilo kulingana na majibu ya wahojiwa wa jinsi ya kike na jinsi ya kiume yalikuwa kama ifuatavyo.

Kielelezo Namba 4.2 Matokeo Kulingana na Jinsi

Namba	Wahojiwa	Ke	Ndiyo	Hapana	Me	Ndiyo	Hapana
1.	Waigizaji	5	5	0	5	5	0
2.	Wanafunzi uigizaji na filamu	15	15	0	15	10	5
3.	Wanafunzi wa fasihi	15	15	0	15	5	10
4.	Hadhira	50	25	0	25	10	15
Jumla		60	60	0	60	30	20

Chanzo: Uchambuzi wa Data za Utafiti, 2013

Ukichunguza kielelezo hicho utaona kuwa wahojiwa wa kike 60 walijibu NDIYO kwa swali hilo na hakuna mhojiwa wa jinsia ya kike aliyejibu HAPANA wakati wanaume 40 walijibu NDIYO na wanaume 20 walijibu HAPANA. Kwa matokeo hayo tnaona kuwa bado pia kuna mvutano baina ya wanawake na wanaume katika kulitazama suala la ujinsia. Katika usaili mhojiwa mmoja alisema,

Wanawake wamekuwa wakijua na kutambua kuwa wanabaguliwa, kugandamizwa na kunyanyaswa na wanaume na wakati huo huowanaume huona kuwa ni haki yao na mwanamke ndivyo anavyotakiwa kuwa katika jamii na si suala la unyanyaswaji bali ni mila na desturi za jamii kuwa mwanamke na mwanaume ni tofauti.

Hivyo basi tunaweza kusema kwamba katika filamu za Kanumba kama kazi zingine za fasihi zinatumia sanaa kumchora mwanamke katika mtazamo hasi ambao ni nafasi aliyopewa katika jamii. Mtazamo huu unatokana na mfumo dume uliopo katika jamii. Kulingana na mfumo dume mwanamke huwa chini ya mwanaume. Wakati wa

majadiliano ya vikundi wahojiwa walitolea mfano wa filamu ya *Johari* katika filamu hiyo mwanamke amechorwa kama chanzo cha matatizo katika jamii. Hapa Kanumba anamweleza mama yake kuwa “si huyu mwanamke mama ameniua mimi ni mfu aliye hai” hapa inaonyesha suala la ukimwi mwanamke ndiye chanzo cha matatizo kwa mwanaume. Tofauti na mwanamke kwa upande mwingine katika filamu hiyo mwanaume amechorwa kama mwenye huruma anayejali maisha ya mtu ambapo Hansi baada ya kujua ana UKIMWI hakutaka kumuambukiza Mainda japo aliweza kuingia nae chumbani lakini alipokumbuka afya yake aliamua kukataa kufanya naye mapenzi wakati msanii hakumpa moyo huo Johari ambaye alimwambukiza Hansi.

Swali lingine lililoulizwa kwa wahojiwa ni; Je kuna mabadiliko yoyote kuhusu nafasi ya mwanamke katika filamu za Kanumba?. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo.

Kielelezo Namba 4.3 Mabadiliko ya Filamu za Kanumba Kuhusu Mwanamke

Namba	Washiriki	Idadi	Waliosema NDIYO	Waliosema HAPANA
1.	Waigizaji	10	0	10
2.	Wanafunzi wa kozi ya filamu na uigizaji	30	0	30
3.	Wanafunzi wa fasihi	30	5	25
4.	Hadhira	50	0	50
	Jumla ya Wahojiwa	120	5	115

Chanzo: uchambuzi wa data, 2013

Ukichunguza matokeo hayo utaona kuwa wahojiwa 115 walijibu Hapana wakati wahojiwa 5 walijibu Ndiyo. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa hakuna mabadiliko

ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Pamoja na harakati za mwanamke kutaka kujikomboa lakini bado kazi za fasihi ambazo zimetungwa katika kipindi hiki hazioneshi mabadiliko ya nafasi ya mwanamke bali humchora katika nafasi hasi tofauti na mwanaume ambaye amekuwa akichorwa katika mtazamo chanya. Matokeo haya hayana tofauti na uchunguzi uliofanywa na Jilala (2010/2011) kwa mashari ya Bongo fleva ambapo mashairi haya ni sanaa pendwa iliyojitokeza miaka ya tisini (Senkoro, 2003; Omari, 2003; Omari, 2010; Jilala; 2008). Kulingana na matokeo ya uchunguzi huo Jilala anaonyesha kuwa wasanii wa mashairi ya bongo fleva humchora mwanmke katika mtazamo hasi tofauti na jinsi ambavyo mwanaume anatazamwa katika jamii. Hivyo tunaweza kusema kuwa bado jamii haijabadilika kuhusu mwanamke na kizazi kilichopita na kilichopo bado mwanamke anatazamwa katika uhasi wake na mwanaume anatazamwa katika uchanya wake. Hata hivyo wasailiwa walikuwa na mawazo yao kuhusu suala la ujinsia ambapo wakati wa usaili mmoja wa wahojiwa alisema kuwa:

Hawa wasanii wa filamu ambao kazi zao si za kusomwa bali kutazamwa kwa macho mtu yeyote mwenye uwezo wa kutazama filamu hizi ana nafasi ya kuzitazama bila kujali kama anajua kusoma au la. Hivyo zinapaswa kuwa na mafundisho ambayo yatarekebisha mielekeo ya jamii hasa suala la mwanmke na mwanaume.

Kwa matokeo hayo tunaweza kusema kuwa ipo haja ya wasanii wa filamu kubadili mielekeo ya jamii kwa kufunza, kuonya na kuadibisha juu ya masuala ya ujinsia katika jamii kwa kuonyesha kuwa hakuna tofauti katika masuala ya kijamii baina ya mwanmke na mwanaume bali tofauti zao ni za kibailojia tu. Kama ilivyoelezwa wakati wa usaili filamu ni sanaa ambayo kila mmoja ana weza kuitazama hata

ambaye hajasoma lakini bado tunaweza kusema kuwa filamu zinaweza zisiwafikie wengi kwa sababu zinahitaji uwezo wa kiuchumi hususani mtu kumiliki televisheni, deki na pia uwezo wa kununua mikanda ya DVD.

4.6 Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke Katika Filamu za Kanumba

Moja ya malengo mahususi ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha nafasi ya mwanamke kama inavyosawiriwa na vipengele vya lugha katika filamu za Steven Kanumba. Katika utafiti huu hadhira ya filamu za Steven Kanumba ambayo ilihusisha watu 50 katika kujibu maswali ya dodoso na usaili na katika majadiliano ya vikundi. Katika kubainisha nafasi ya mwanamke katika filamu za Steven Kanumba matokeo yalikuwa kama ifuatavyo;

Kielelezo namba 4.5 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Namba	**Nafasi ya Mwanamke**
1.	Mwanamke kama mama
2.	Mwanamke kama chombo cha starehe
3.	Mwanamke kama kiumbe dhaifu
4.	Mwanamke kama kiumbe kisichokuwa na maamuzi binafsi
5.	Mwanamke kama kiumbe tegemezi
6.	Mwanamke kama chanzo cha matatizo
7.	Msaliti asiyekuwa na msimamo

Chanzo: Data za utafiti, Januari, 2013

Kielelezo hicho kinaonyesha nafasi za mwanamke zinazojitokeza katika filamu za Kanumba kama zilizobainishwa na wahojiwa wakati wa majadiliano ya vikundi. Iligundulika katika filamu hizo mwanamke anachorwa kama mama, chombo cha satrehe, kimue dhaifu, kiume kisichokuwa na maamuzi binafsi, kiumbe tegemezi, chanzo cha matatizo na msaliti asiyekuwa na msimamo. Sehemu ifuatayo inaelezea matokeo hayo kwa mifano kutoka katika filamu.

4.6.1 Mwanamke Kama Mama

Katika utafiti huu iligundlika kuwa filamu za Kanumba humchora mwanamke kama mama na mwanamke kama mama hupewa lugha ambayo inamsifia katika nafasi hiyo ambayo ni tofauti na jinsi ambavyo mwanamke anachorwa katika nafasi zingine. Kwa mfano katika filamu ya Johari lugha anayoitumia mhusika Hansi kumwelezea mama ni tofauti na lugha anayoitumia kumwelezea Johari. Aidha mama anachorwa kama mwenye huruma na upendo kwa watoto na hata Hansi anapogundua ana UKIMWI anamlilia mama yake bila kujali kuwa; Yeye ni mwanaume. Ilielezwa katika majadiliano ya vikundi na usaili kuwa

"Mwanamke anaposimama kama mama huwa ni tofauti na mwanamke kama mpenzi ama mke. Hivyo mwanamke kama mama ana nafasi kubwa katika jamii nimungu wa pili".

Mmoja wa wahojiwa wakati wa majadiliano ya vikundi alieleza kuwa;

Mimi nikiwa na kitu kinachoniuma zaidi, kinanitatiza hasa namkimbilia mama yangu si rahisi kwenda kwa baba.

Kwa matokeo hayo tunaona kuwa mama ana nafasi kubwa sana katika jamii, mwanamke kama mama ni msiri, mfariji, mshauri, mlezi, msimamizi, mwenye upole, mwenye upendo, huruma na mapenzi ya dhati kwa watoto. Katika Johari mwanamke amechorwa kama mshauri, mlezi, na mwenye huruma na upendo wa dhati kwa watoto. Mfano mama anatumia tamathali za semi kutoa mafunzo kwa mwanawe kama ifuatavyo;

i) Kumbuka mwanangu dunia hadaa ulimwengu shujaaa,

ii) Epuka kuyumbishwa na dunia.

iii) Mchumia juani hulia kivulini

iv) Mwanzo wa mapenzi huwa matamu kama asali na mwisho ni machungu kama shubiri.

Ukichunguza maneno hayo utaona kuwa lugha anayotumia mwanamke kama mama ni lugha inayotoa mafunzo, kuonya na kuadibu kwa watoto. Ni lugha inayoonyesha nafasi yake katika jamii kama mlezi, mshauri, mzazi na mwenye wajibu mkubwa kwa watoto na jamii kwa ujumla. Akiongelea nafasi ya mwanamke kama mama katika nyimbo za kizazi kipya, Jilala (2008) anasema sitiari zinazotumika katika nyimbo za kizazi kipya humchora mwanamke kama mama na sitiari hizo huwa ni tofauti na zile zinazomchora mwanamke kama mpenzi ama vinginevyo. Kwa mfano sitiari zinazotumika kumwelezea mama ni *nguzo*, *taa*. Tofauti na zile zinazomwelezea mpenzi kama vile mtoto, malaika, uwaridi, kopo lenye marashi (Jilala, 2010/2011).

Kwa matokeo haya tunaweza kusema kuwa mwanamke anapokuwa mama huwa na nafasi kubwa katika jamii tofauti na mwanamke anapotajwa kama mke, mpenzi ama mchumba huonekana ni kiumbe dhaifu, tegemezi, chombo cha starehe kwa mwanamume. Hivyo basi, hii inaonyesha kuwa mwanamke anapochorwa kama mama katika kazi za fasihi hupewa nafasi chanya na kuonyesha nguvu yake katika kujenga na kuongoza familia hususani katika malezi ya familia. Kwa maana hiyo mifano hii inaonyesha kuwa si mara zote mwanamke huchorwa kama katika uhasi bali hutegemea na mahusiano ya kijamii yaliyopo.

4.6.2 Mwanamke Kama Chombo cha Starehe

Utafiti huu uligundua kuwa katika filamu za Kanumba mwanamke amechorwa kama chombo cha starehe. Mwanamke amechorwa kama chombo cha kumstarehesha mwanaume pale anapomhitaji. Kwa mfano kwa kutumia lugha ya kejeli na dhihaka Moses anamwambia katibu muhtasi wake kuwa *"leo jioni uje nyumbani nakuhitaji"* bila kipingamizi mwanamke anajibu "sawa" ukitazama filamu hiyo Misose anaongea kwa dharau na kujiamini ikiwa ni kauli ya shuruti wakati mwanamke anaonekana mnyenyekevu na mwenye hofu na wasi wasi.

Katika filamu ya Moses utaona kuwa, msanii amemchora Moses akiwa mwenye kuwatumia wanawake pale anapopenda bila kujali thamani ya utu wao. Kwa mfano dada yake

"Anamwambia ina maana kaka wanawake wote unaotembea nao unawatumia kwa haja zako tu?" Moses anajibu *"ndiyo kwa sababu ni wajinga wapumbavu hawana akili"*

Nukuu hiyo inadhihirisha kuwa mwanamke anatumiwa kama chombo cha kumstarehesha mwanaume. Suala hili linadhihirshwa pia na kauli ya mpenzi wa Moses mwanamke anasema

"*Ina maana nia yako ilikuwa ni kunitumia tu halafu basi".*

Katika filamu ya Johari tunamuona Ray akisema

"Nawatumia wanawake na ipo siku watakuja wakilia na kunikumbuka, wao ni pesa tu, pesa zangu ndizo zinazowavuta"

Kauli ya Johari pia inathibitisha hilo anasema;

"Ulikuwa unanitumia tu kwa starehe zako hukuwa na mapenzi na mimi"

Kwa mifano hiyo, tunaona kuwa mwanamke amechorwa kama chombo cha kumsarehesha mwanaume na mwanaume anamtumia mwanamke kwa haja zake. Hii inaonekana pia katika Johari ambapo Jack anaonekana ni mwanaume anayewatumia wanawake bila kujali tahamni yao, kuwalaghai na kuwatumia kwa starehe zake na hatimaye anawaambukiza UKIMWI huku akiona ni haki yao. Kwa mfano Jack *"anasema ni tamaa zao kupenda wanaume wenye magari, majumba ya kifahari, pesa bila kujua vyote hivyo vimepatikana wapi"*

Anaongeza *"Nina nyumba nzuri, gari zuri, na nina pesa wanawake wengi wamekuwa wakitamani kuwa na mimi bila kujua pesa nimezipata wapi"*

Aidha mwanamke amechorwa kujiamini katika nafasi hiyo kwa kujiona yeye ni chombo cha kumstarehesha mwanaume pindi anapomhitaji. Hivyo basi, mwanamke anatumia nafasi yake kumstarehesha mwanaume. Kwa mfano katika filamu ya Johari mwanamke anamwambia Jack

"Nikupe penzi gani ulidhike ili usitoke nje"

Hapa mwanamke anaonekana kuamini kuwa yeye ndiye anapaswa kumfanya mwanaume asiwe na wapenzi wengi na yupo kwa ajili ya kumridhisha mwanaume. Wakati wa majadiliano ya vikundi, wahojiwa walieleza kuwa mwanamke anaamini kuwa anapaswa kumstarehesha mwanaume na anapaswa kutumia nafasi hiyo ili kumpa starehe mwanaume. Imeelezwa na watafiti wengine kuwa wanawake huamini

katika nafasi ambayo wamelelewa na kukua wakiifahamu kama nafasi yao katika jamii na huishi kwa kufuata nafasi hiyo (Mutembei, 2010; Momanyi, 2003; Jilala, 2008 na 2010/2011; Mnenuka, 2010/2011)

4.6.3 Mwanamke Kama Kiumbe Dhaifu na Tegemezi

Katika utafiti huu ilibainika kuwa mwanamke anachukuliwa kama kiumbe dhaifu. Udhaifu wa mwanamke umejengeka katika kazi na mapenzi. Kwa mfano katika filamu ya Johari, msanii amemchora Johari kama kiumbe dhaifu katika mahusiano, pamoja na kuwa haonyeshwi mapenzi ya dhati na Ray lakini bado anaonekana kumfuata na kumuonyesha kumpenda. Aidha Mainda anaonekana kulilia penzi la Hansi na kumtaka awe mpenzi wake. Kwa upande mwingine Ray anatumia pesa kama ishara ya silaha ya kumpata kila mwanamke anayemtaka na hivyo anaonekana kwa silaha ya pesa anawapata wanawake wengi na hatimaye kuwaambukiza UKIMWI. Hili pia linathibitshwa na kauli ya Moses katika filamu ya Moses, kwa mfano anasema;

i) “Nyie wanawake ni watu wa ajabu sana unataka mwanaume ndiyo afikirie mustakabali wa maisha yako huo ni ujinga”
ii) “Ama kweli nyie wanawake mnavichwa vya kuku”
iii) “Wanawake ni kuku, kuku kabisa wa kulia ko ko ko”
iv) “Vichwa vya kuku hakuna kitu women chicken”

Kwa mifano hiyo tunaona kuwa mwanamke amechorwa kama kiumbe dhaifu asiye na akili wa uwezo wa kufanya jambo lolote katika jamii. Mwanamke amechorwa kama mtu asiyejitambua wala uwezo wa kufanya maamuzi juu ya maisha yake

binafsi. Akili ya mwanamke inafananishwa na akili ya kuku. Hii inaonyesha mwanamke hawezi kufanya jambo lolote hawezi kujitegemea hawezi kufanya maamuzi kwa mfano namba (iv) anaposema “vichwa vya kuku hakuna kitu women chicken” inaonyesha kuwa mwanamke hana mawazo, akili wala fikra kichwani.

Mifano hii inamdharirisha mwanamke kwa kumuonyesha kuwa ni kiumbe tegemezi asiye na maamuzi kichwani. Mfano namba (i) msanii anajaribu kuuweka wazi msimamo na mtazamo wake kuhusu mwanamke kuwa wanategemea wanaume wafikiri kwa ajili yao. Hii inadhihirisha kuwa msanii anamtazama mwanamke kama kiumbe amabye ni tegemezi kimawazo, kifikra na maamuzi.

Utafiti huu uligundua kuwa katika filamu za Kanumba mwanamke anachorwa kama kiumbe tegemezi ambaye hawezi kusimama bila nguzo ya mwanaume. Wakati wa usaili na majadiliano ya vikundi wahojiwa walibainisha kuwa mwanamke amechorwa kama kiumbe tegemezi kwa kutumia lugha ya picha mfano katika Moses anamfananisha mwanamke na paka. Anasema:

Kumfundisha mwanamke ni sawa na hadithi ya muuza kahawa na paka wake sayona ambaye alijitapa kumfundisha kila kitu na alipomtuma alitekeleza akawa anawaonyesha wateja wake jinsi alivyompa mafunzo paka wake na akimtuma kufanya jambo anafanya na akimzuia anatekeleza. Mteja mmoja akamweka panya chini mara Yule paka akasahau maagizo ya bosi wake na kumfata panya. Hivyo inaonyesha mwanamke ni mwanamke tu hata ukimfundisha atabaki kuwa na tabia za kike tu.

Kwa mfano huu inaonyesha mwanamke ni tegemezi kwa mwanaume pamoja na utegemezi huo lakini bado ni kiumbe ambaye hawezi kusimama yeye kama yeye na hata hivyo ni kiumbe ambaye habadiliki na anasimama katika nafasi aliyopewa katika jamii. Utafiti huu umegundua kuwa lugha imetumika kumdhalilisha mwanamke na kuonyesha kuwa mwanamke ni kiumbe duni na tegemezi.

4.6.4 Mwanamke Kama Kiumbe Kisichokuwa na Maamuzi Binafsi

Katika utafiti huu iligundulika kuwa mwanamke anachorwa kama kiumbe kisichokuwa na maamuzi binafsi. Mwanamke anaonekana hawezi kuamua bila uwepo wa mwanamume. Hawezi kufanya kazi na kuleta ufanisi katika kazi bila kuwa na mwanaume. Kwa mfano ilielezwa katika majadiliano ya vikundi kuwa katika filamu ya Moses neno "she is a woman' lina ashiria kuwa mwanamke ana sifa zake mwanamke ni kiumbe ambaye hawezi kusimama peke yake bila kuwa na mwanaume. Hata katika harakati za kuinusuru kampuni katika filamu ya Moses, msanii anaonyesha kushindwa kwa Stela na mapendekezo yanayotolewa na Moses yanaonekana kuwa ndiyo sahihi na yanatumiwa katika kujenga kampuni. Moses anasema:

She is a woman, ni mwanmke tu tangu lini mwanamke akawa na maamuzi sahihi? Wanawake hawako serious na mambo wanayoyafanya, wanawake wanapokaa wanazungumza habari za wanaume tu hawana issue zingine wanazoziongea zaidi ya wanaume.

Maneno haya yanajenga picha kuwa mwanamke ni kiumbe asiyekuwa na maamuzi yake binafsi na hawezi kusimama bila mwanaume. Hii inadhihilisha kuwa lugha

iliyotumika katika filamu za Kanumba zinamchora mwanamke kama kiumbe asiye na maamuzi juu ya maisha yake na maendeleo.

4.6.5 Mwanamke Kama Chanzo cha Matatizo

Utafiti huu umegundua kuwa mwanamke anachukuliwa kama chanzo cha tatizo. Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walitaja filamu ya My Valentine kuwa inaonyesha kuwa mwanamke ndiye chanzo cha tatizo la kukosa mtoto katika familia. Mfano inaonyesha Kanumba akiamua kutafuta mwanamke mwingine baada ya kuona mkewe hapati mtoto. Mkewe anasisitiza

"*Twende tukapime mume wangu tujue nini tatizo*, mume anajibu *nenda wewe maana ndiye unatakiwa kujua tatizo ni nini!"*

Mwanaume anasema *"Kwa nini huzai"*. Kauli hii ya mwanamme inadhihirisha kuwa katika suala la uzazi mwanamke ndiye ana jukumu la kuzaa na si jukumu la mume na mke. Familia isipopata mtoto jamii inatupia lawama kwa mwanamke na mwanamke anaonekana kuwa ndiye mwenye hatia. Aidha matokeo yanaonyesha kuwa thamani ya mwanamke ni kuzaa. Kwa mfano katika filamu ya My Valentine Kanumba anaonekana kutafuta mwanamke mwingine baada ya kuona kuwa mke wake hazai. Anapodanganywa kuwa huyu kimada ana mimba yake Kanumba anaonyesha furaha ya ajabu na kumthamini mwanamke huyo hata kusahau ndoa yake na kumdharau mkewe. Hii pia inadhihirishwa na kitendo cha Kanumba kurudi kwa mke wake baada ya huyo mwanamke kuzaa mtoto ambaye si wake (mtoto wa Kizungu).

Aidha jamii pia inaonekana kumlaumu mwanamke kuwa hazai na mwanamke asiye zaa hajui uchungu wa mtoto. Kwa mfano tunaona familia ya mtoto aliyepigana na mwenzie shuleni lakini lawama za wazazi zinarudi kwa mke wa Kanumba ambaye hajazaa. Unajua uzazi wewe? Hivyo basi, katika suala la uzazi mwanamke anaonekana ndiye mwenye makosa na ni chanzo cha matatizo ya kutokuzaa wakati mwanaume yeye anaonekana ni salama. Imeelezwa na watafiti wengine kuwa katika jamii za Kiafrika mwanamke huonekana kuwa ni chanzo cha matatizo katika jamii (Kisekka, 1990; Schiapper, 1991) vile vile katika kuelezea tatizo la UKIMWI, (Mutembei, 2009; Omari, 2012 na Jilala, 2010/2011) wanaeleza kuwa mwanamke huonekana ndio Chanzo cha tatizo la UKIMWI katika jamii wakati mwanamke akionekana ni chanzo cha tatizo hilo na ndiye aliyeuleta. Katika filamu ya Johari tunamuona Hansi akimshutumu Johari baada ya kugundulika kuwa na UKIMWI anasema *umeniua kwa makusudi* huku akimpiga. Wakati huo Johari akilia na kulalamika *unanishutumu bure me sijui kitu!* Kwa mfano huu tunaona kuwa lawama anatupiwa mwanamke bila kujali kuwa yeye pia ana nafasi gani na mwanaume ana nafasi gani. Aidha katika filamu hiyo pia mama yake Hansi anamlilia Johari

"Nikubebee mbeleko gani? Kwa nini umeamua kuangamiza familia yangu? Unaniulia mwanangu? Ulikosa nyumba ya kuupeleka huo UKIMWI ukaona uulete kwangu?"

4.6.5 Mwanamke Kama Msaliti

Mwanamke anachorwa kama msaliti wa mapenzi na msaliti wa familia hasa anapokuwa katika mahusiano ya mapenzi. Kwa mfano katika "she is my sister' mwanamke amechorwa kuwa ni msaliti anayeweza kuvunja ndoa ya mtu kwa

kutumia ulaghai wa mapenzi. Katika *unachangia Dan, unaniweka gizani, frola and Dan are having an affair.* Hapa msanii anaonyesha kuwa mwanamke ana uwezo wa kumsaliti rafiki yake na kutembea na mumewe mradi awe na pesa. Frora anaonekana tangu awali kutokumpenda Dan na kumshawishi Rose amwache. Utawezaje kuishi na huyo mshamba? Lakini baada ya Dan kupata pesa na kuonekana ana pesa Frola anamlaghai na kuiba penzi la mume wa rafiki yake. Kwa mfano Frola anasema "tell this rubbish to go! I feel like vomiting, I feel like dying!"

Rose anasema "Frola you are taking my husband and everything I own"
Kwa mifano hiyo tunaona kuwa mwanamke anachorwa kama msaliti na mwizi wa mapenzi. Aidha mwanamke anaonekana ni msariti katika ndoa na anapokuwa katika usariti anakuwa hana mapenzi ya familia na watoto. Katika filamu ya Moses mama yake Moses anasema:

Nyie panya, nawachukia wewe na hiyo mipanya yako, najuta kuzaa na mwanaume kama wewe, nakuchukia unaniganda kama ruba.

Kwa mifano hiyo tunaona kuwa mwanamke amechorwa kama msaliti na asiyekuwa na chembe ya huruma kwa familia. Wakati wa majadiliano ilielezwa kwamba mwanamke amechorwa kama kiumbe katili na asiye na uchungu na familia yake. Mwanamke anaonekana ni mnyanyasaji katika suala la mahusiano ya kimapenzi na msaliti.

4.6.6 Mwanamke Kama Kiumbe Mvumilivu na Mnyenyekevu

Mwanamke amechorwa kama kiumbe mvumilivu, mwenye huruma na mnyenyekevu. Kwa mfano katika majadiliano ya vikundi wahojiwa walitaja filamu

ya Johari ambapo Johari amechorwa kama mwanamke ambaye ni mvumilivu na mwenye mapenzi ya dhati ambaye ameweza kumvumilia Jack mwanaume ambaye hakuwa na upendo wa dhati bali penzi la ulaghai lenye lengo la kuambukiza UKIMWI. Johari anasema:

"Nimevumilia sana, kila siku majukumu! Majukumu! Majukumu!

Pia Johari anaonekana mwenye kunyenyekea na kuomba samahani hata pale anapokosewa yeye bali anapiga goti na kuomba samahani. Hii inaonekana pia katika Moses ambapo Joyce anapeleka ua kama ishara ya upendo lakini Moses anatukana na kumfukuza. Joyce anaonekana pia akiomba msamaha kwa kosa la kumletea mpenzi wake Moses maua. Hii inaonyesha kuwa wanawake wamechorwa ni wenye upendo wa dhati lakini pia ni wavumilivu na wanyenyekevu kwa wanaume. Pamoja na unyeyekevu wa mwanamke, mwanaume anaonekana kuwa na lugha kali na isiyo na unyenyekevu kwa mke wake.kwa upande mwingine lugha inayotumiwa na mwanamke katika filamu ya *My Valentine* ni lugha ya unyenyekevu na uvumilivu. Mke wa Kanumba anasema "Mume wangu basi tukae tuzungumze nakuomba mume wangu tujue tatizo ni nini na kwa nini hatupati mtoto" Kanumba anajibu kwa ukali sana "kaa mwenyewe huo muda sina! Nina shughuli za kufanya kila siku watoto unawazalia chooni tu na kujaza choo"

4.7 Tofauti ya Mwanamke na Mwanaume Katika Filamu za Kanumba

Utafiti huu umegundua kuwa katika filamu alizotunga Kanumba kuna mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume. Tofauti ya mahusiano haya imejengeka katika misingi ya kijamii ambapo tangu awali jamii inawaona tofauti. Mfano katika

filamu ya *Moses*, Moses anafungua tofauti hizo baina ya mwanamke na mwanaume kwa kusema:

"When a boy is born the treatment of making him a perfect man starts from there! But if it is a girl they start to call her those weak names; queen, adurable, angle, beautiful those are weak names lakini mwanaume utasikia akiambiwa be a man, stop crying like a girl, stop crying like a woman, wewe ni mwanaume. Hata wanawake wakifanya jambo kubwa huambiwa we ni mwanaume kweli!"

Kwa lugha hii ambayo imetumiwa na mhusika Moses inaonyesha tofauti iliyopo baina ya mwanaume na mwanamke katika jamii. Lugha ambayo yanatumiwa kumrejelea mwanamke huwa ni tofauti na lugha inayotumiwa kumrejelea mwanaume. Matokeo haya hayapo tofauti na matokeo ya Jilala (2010/2011) katika uchunguzi wake wa mashairi ya bongo fleva ambapo alisema kuwa sitiari ambazo zinamrejelea mwanamke zimebeba dhana tano ambazo ni thamani, unyenyekevu, utamu na mvuto wakati mwanaume hubeba taswira ya uhodari, ushujaa, na mwenye maamuzi binafsi. Hivyo basi, mwanamke anakua kulelewa katika utamaduni unaomjenga kuwa ni kiumbe dhaifu na duni ukilinganisha na mwanaume (Momanyi, 2002).

Hivyo basi, tunaweza kusema ku wanamke na mwanaume katika filamu za Kanumba wamechorwa katika mahusiano tofauti ya kijamii, katika suala la mapenzi, katika suala la ndoa, katika suala la madaraka na uongozi. Kwa mfano, wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walitolea mfano, filamu ya Moses ambapo msanii amempa udhaifu na kumuonyesha mwanamke ni dhaifu kuliko mwanaume katika

uongozi na madaraka. Mfano Moses anapomwambia bosi wake kuwa:

"*unatakiwa kuwa makini sana unapowapa wanawake madaraka, una imani na Judice? She is a woman".*

Maneno yaliyotumika hapo yanaonyesha kuwa mwanamke si kiumbe wa kutegemewa na kuaminiwa kulingana na mawazo ya msanii. Katika majadiliano ya vikundi wahojiwa walieleza kuwa lugha iliyotumika katika sentensi hiyo inaonyesha jinsi gani mwanamke anachukuliwa katika jamii. Nafasi anayopewa ni ya udhalilishaji, unyanyasaji na ukandamizaji. Mwanamke anaonekana hawezi kufanya kazi za uongozi wala kuaminiwa katika maendeleo ya nchi.

4.8 Hitimisho

Sura hii imejadili juu ya uwasilishaji wa data na uchambuzi wa data. Katika sura hii vipengele vya lugha ambavyo vinajitokeza katika filamu za Kanumba zilizoteuliwa kufanyiwa uchunguzi vimebainishwa ambapo imeonekana kuwa kejeli na dhihaka ndiyo kipengele kinachotumika zaidi katika filamu hizo. Wahojiwa walipoulizwa juu ya sababu ya kujitokeza zaidi kwa kejeli na dhihaka. Walieleza kuwa matumizi ya dhihaka humsaidia mtu kuibua mambo mazito na kuyawasilisha katika jamiii bila hofu wala wasiwasi. Hivyo basi kwa matokeo hayo tunaona kuwa katika filamu zilizotungwa na Kanumba kejeli na dhihaka ndiyo lugha ambayo imetumika zaidi kama mbinu ya kisanii kwa lengo la kufikisha ujumbe katika jamii husika. Aidha sura hii imejadili kuwa vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba vinatumika kuwasilisha mahusiano ya kijinsia baina ya mwanamke na mwanaume ambapo lugha inayotumika kumwelezea mwanamke ni tofauti na lugha inayotumiwa kumwelezea

mwanamme. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa, mwanamke na mwanaume katika filamu za Kanumba wamechorwa katika mahusiano tofauti ya kijamii, katika suala la mapenzi, katika suala la ndoa, katika suala la madaraka na uongozi. Mwanamme anaonekana kuwa ni jasiri ambaye anaweza kutoa maamuzi na kubadilika wakati mwanamke anaonekana kuwa ni kiumbe ambaye hawezi kuwa na maamuzi binafsi na uwezo wa kubadilika. Katika filamu za Kanumba mwanamke amechorwa kama kiumbe duni, kiumbe asiyekuwa na maamuzi binafsi, tegemezi, msaliti na asiyefaa kupewa madaraka ya aina yoyote katika jamii. Sura hii imejadili kuwa usawiri wa nafasi ya mwanamke katika filamu za Kanumba umejikita katika kumtazama mwanamke katika nafasi ya Mwanamke kama mama, Mwanamke kama chombo cha starehe, Mwanamke kama kiumbe dhaifu, Mwanamke kama kiumbe kisichokuwa na maamuzi binafsi, Mwanamke kama kiumbe tegemezi, Mwanamke kama chanzo cha matatizo, Msaliti asiyekuwa na msimamo. Sura hii imejadili kuwa hakuna mabadiliko ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Pamoja na harakati za mwanamke kutaka kujikomboa lakini bado kazi za fasihi ambazo zimetungwa katika kipindi hiki hazioneshi mabadiliko ya nafasi ya mwanamke bali humchora katika nafasi hasi tofauti na mwanaume ambaye amekuwa akichorwa katika mtazamo chanya.

SURA YA TANO

5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo inatoa muhtasiri, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inaelezea muhtasari wa matokeo ya utafiti huu, sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa kijinsia katika lugha ya filamu za Steven Kanumba ili kuona ni jinsi gani lugha inatumika kusawiri masuala ya kijinsia katika jamii. Utafiti huu una malengo mahususi manne ambayo ni: Kubainisha vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba, Kujadili jinsi vipengele vya lugha vilivyobainishwa vinavyosawiri mahusiano ya kijinsia baina ya wanawake na wanaume, Kujadili nafasi ya mwanamke kama inavyosawiriwa na vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba na Kujadili sababu za uteuzi wa lugha katika kusawiri masuala ya kijinsia. Utafiti huu ulikusudia kujibu maswali yafuatayo; Ni vipengele vipi lugha vinavyotumika katika filamu za Kanumba? Je, vipengele vya lugha vilivyobainishwa katika filamu za Kanumba vinasawiri vipi mahusiano ya kijinsia baina ya wanawake na wanaume? Je, nini nafasi ya mwanamke kama inavyosawiriwa na vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba? Je, ni kwa nini uteuzi wa lugha ya namna fulani hufanyika katika kusawiri masuala ya kijinsia?

Utafiti huu ulifanyika maktabani na katika maeneo teule ambayo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuwahoji wanafunzi wa fasihi. Tulichagua maktaba na maeneo yaliyoko Dar es Salaam kwa kuzingatia kuwa mji wa Dar es Salaam una taasisi na wapenzi wengi wa filamu ambazo hivi sasa zinajulikana kama *Bongo Movies.* Aidha utafiti huu uliwahoji wazalishaji wa filamu waliopo Dar es salaam na waigizaji ambao walifanya kazi ya kuigiza filamu na Kanumba.

Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha wazi kuwa filamu za Kanumba zimetumia lugha kwa namna ambayo inasawiri mahusiano ya kijinsia katika jamii mbalimbali hususani jamii ya Watanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla kama eneo asilia linalozungumza na kumiliki fasihi ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa Kanumba katika filamu zake ametumia zaidi kejeli na dhihaka kuliko vipengele vingine vya lugha. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirsha kuwa kejeli na dhihaka ndiyo mbinu ya kifani inayomtabulisha Steven Kanumba katika upekee wake wa kisanii. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa kuna sababu ambazo zilimfanya Steven Kanumba kutumia kejeli na mbinu nyingine za kifani kwa njia ya matumizi ya pekee ya lugha. Taarifa za utafiti zimeonesha kuwa sababu za kutumia tamathali za usemi kama vile kejeli na dhihaka zilitokana na uwezo wake wa kusaidia kuibua masuala mbalimbali mazito ya kijamii bila hofu na wasiwasi. Hivyo, tamathali ni njia ya kuepukana na udhibiti wa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Utafiti huu umedhihirisha kuwepo kwa usawiri wa mwanamke kwa namna mbalimbali. Katika kazi za fasihi za Kanumba imedhihirika kwamba mwanamke anasawiriwa kama mama, chombo cha starehe, kiumbe dhaifu na tegemezi, kiumbe

kisichokuwa na maamuzi binafsi, chanzo cha matatizo, msaliti, na ni kiumbe mvumilivu na mnyenyekevu.

Vilevile mtafiti alibaini kuwa filamu za Kanumba zinaonesha tofauti iliyopo baina ya mwanamke na mwanaume katika jamii. Utafiti huu umegundua kuwa katika filamu alizotunga Kanumba kuna mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume. Tofauti ya mahusiano haya imejengeka katika misingi ya kijamii ambapo tangu awali jamii inawaona wanaume ni tofauti na wanawake. Hata wanawake wakifanya jambo kubwa huambiwa we ni mwanaume kweli! Kwa lugha hii ambayo imetumiwa na mhusika Moses inaonyesha tofauti iliyopo baina ya mwanaume na mwanamke katika jamii. Aidha, utafiti huu umebaini kuwa lugha ambayo inatumiwa kumrejelea mwanamke huwa ni tofauti na lugha inayotumiwa kumrejelea mwanaume. Lugha inayotumiwa kumrejelea mwanamke hutumia maneno yenye kurejelea vitu vya thamani, urembo, uzuri, utamu tofauti na lugha inayotumika kumrejelea mwanamme huwa inahusisha vitu vyenye uhodari, uwezo na nguvu. Hivyo basi, utafiti huu unakubaliana na tafiti zingine kuwa lugha inayotumika kumrejelea mwanamke ni tofauti na ile inayotumika kumrejelea mwanaume na mwanamke na anakua na kulelewa katika utamaduni unaomjenga kuwa ni kiumbe dhaifu na duni ukilinganisha na mwanaume (Jilala, 2010/2011; Mutembei, 2010).

Hivyo basi tunaweza kusema kuwa, mwanamke na mwanaume katika filamu za Steven Kanumba wamechorwa katika mahusiano tofauti ya kijamii, katika suala la mapenzi, katika suala la ndoa, katika suala la madaraka na uongozi. Kwa mfano, wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walitolea mfano filamu ya Moses

ambapo msanii amempa udhaifu na kumuonyesha mwanamke ni dhaifu kuliko mwanaume katika uongozi na madaraka. Mfano Moses anamwambia bosi wake kuwa, "*unatakiwa kuwa makini sana unapowapa wanawake madaraka, una imani na Judice? She is a woman"* Maneno yaliyotumika hapo yanaonyesha kuwa mwanamke si kiumbe wa kutegemewa wala kuaminiwa kulingana na mawazo ya msanii. Neno she is a woman linaashiria jinsi mwanamke anavyochorwa katika jamii. Kiumbe duni, asiye na maamuzi, asiyeweza kuongoza wala kushika madaraka ya kuongoza jamii.

5.3 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, utafiti huu umegundua kuwa, tamathali za semi hutumika katika kusawiri masuala ya kijiinsia katika filamu za Steven Kanumba. Utafiti huu umegundua kuwa mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume yanaelezewa kupitia tamathali za semi na hivyo tamathali za semi hutumika kumchora mwanamke tofauti na jinsi zinavyotumika kumchora mwanaume. Mwanamke huchorwa kama kiumbe dhaifu, tegemezi na asiye na maamuzi binafsi ambaye anapaswa kumnyenyekea na kumtii mwanaume. Aidha mwanaume amechorwa kama kiumbe shupavu, jasiri, hodari na mwenye maaumuzi binafsi katika jamii,. Mwanaume anaonekana hata katika dini ana maamuzi na mamlaka juu ya mwanamke. Hivyo lugha kupitia kipengele cha tamathali za semi huonyesha mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanamme. Utafiti huu umedhihirisha kuwa mwanamke anapewa nafasi tofauti na mwanaume ambazo zinadhihirishwa kupitia kipengele cha tamathali za semi. Mfano Kwa kutumika tamathali za semi nafasi ya mwanamke inajibainisha katika: asasi ya ndoa, kufanya maamuzi, elimu,

uzazi na malezi, mapenzi, utamaduni, dini na mwanamke kama kiumbe muhimu katika jamii.

Aidha, utafiti huu umechangia katika kuongeza maarifa mapya katika taaluma ya fasihi hususan katika uwanja wa filamu za Kiswahili katika kubainisha nafasi ya tamathali za semi katika kusawiri masuala mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na mahusiano baina ya wanawake na wanaume. Hii ni kwa sababu utafiti huu umebainisha aina za tamathali za semi zinazotumiwa katika mashairi ambayo pia ni tamathali ambazo hutumiwa katika mawasiliano ya kawaida ndani ya jamii. Matokeo ya utafiti huu yatawasaidia wataalamu wengine wa fasihi kuweza kujua imani, hisia, mtazamo, maoni, matatizo na falsafa ya Waswahili inayodhihirishwa na tamathali za semi.

Vilevile ni rahisi kuwasaidia kutatua matatizo yanayowakabili wazungumzaji wa Kiswahili baada ya kuelewa dhima na nafasi ya tamathali za semi katika kusawiri mahusiano ya kijinsia. Kwa kuelewa ujumbe unaopatikana katika tamathali za semi ni rahisi kusaidia kuondoa mitazamo potofu na miundo ya kiutawala inayowanyima fursa watu wengine wa kundi fulani kushirika katika mipango ya maendeleo na kuwa sehemu ya maamuzi hayo.

Kwa ujumla tumebaini kuwa filamu za Kiswahili zinafumbata amali mbalimbali za kijamii na kwamba kupitia filamu za Kiswahili tunaweza kugundua mahusiano yasiyofaa baina ya jinsia zote mbili. Hivyo, ili tuweze kuondoa unyanyasaji wa wanawake ni vema kutunga filamu zinazokataza vitendo vyote vinavyomdhalilisha

mwanamke na kukwamisha maendeleo yake kwa namna mbalimbali. Matumizi ya lugha yajikite katika kuleta usawa wa kijinsia kusiwe na lugha ya mwanamke na lugha ya mwanaume.

5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umechunguza matumizi ya lugha katika filamu za Kanumba na namna vinavyosawiri suala la ujinsia kwa kuonyesha nafasi ya mwanamke na mahusiano tofauti baina ya mwanamke na mwanaume. Utafiti huu unapendekeza kuwa bado kuna haja ya jamii kutunga filamu ambazo zinaonyesha haki sawa kwa mwanamke na mwanaume ili kujenga jamii yenye usawa wa kijinsia. Aidha, utafiti huu unapendekeza kuwa lugha inayotumika katika kazi za sanaa ambazo zinatazamwa na kusikilizwa na jamii zitumie lugha inayohimiza usawa wa kijinsia. Lugha ziwe sawa na baina ya mwanamke na mwanaume ili kulinda haki za kijinsia.

Utafiti huu unapendekeza tafiti zijazo zijikite katika kuchunguza na kulinganisha matumizi ya lugha katika kazi za kipindi kimoja na za vipindi tofauti ili kuchunguza maendeleo ya filamu za Kanumba

MAREJEO

Alderson, C.G. & Beretta, A. (1992). (Wah.) *Evaluating Second Education: Cambridge applied linguistics*, C.U.P.

Babbie, E (1992). *The Practice of Social Research*. 6th edition. Wadsworth Publishing Company.

Bachman, R. & Schutt, R. (2007). *The practice of research in criminology and criminal justice*

Baker, T. (1994). *Doing social research*. Singapore: McGraw-Hill.

Belk, W.R. (2006). Handbook of Qualitative Research Methods in Marketing. Toronto: *Kraft Foods Canada Chair of Marketing.* Schulich School of Business, York University.

Berg, B. L. (2004). *Qualitative Research Methods for the Social Science.* (Toleo la 5.).

Boston: Pearson Education, Inc.

Best and Kahn, J. (1993). *Research in Education*. New York: Allyn Bacon Inc.

Birihanze, J. N. (1971). "African Theatre, Call for a Change". UMMA Journal Vol 2. Dar es Salaam: DUP.

Borg, W.R and Gall, M.D, (2003). *Educational Research: An Introduction***.** Longman London.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (2nd edition). Oxford: Oxford University Press.

Cham, M. B. (1999). "African Cinema" An Essay prepared for WORLD CULTURE REPORT, UNESCO

Cohen, L, Manion, L and Morrison, K (2000). *Research Methods in Education*. 5th edition. London: Rutledge Falmer.

Daymon, C. and Holloway, I. (2002). *Qualitative Research Methods in Public Relations and Marketing Communications*. London: Routledge.

De Vaus, D. A. 1993. *Surveys in Social Research* (Toleo la 3.). London:UCL Press

Diawara, M. (1992). *African Cinema: Politics and Culture.* Bloomington: Indian University Press.

Holloway, L. (1997). *Basic Concepts for Qualitative Research*. Oxford: Blackwell Science.

Inyani, S.K. (2002). Utafiti wa Kiswahili na Maswala ya Uana: UTAFITI WA KISWAHILI. Nairobi. Downtown Printing Works ltd

Jilala, H. (2008). 'The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania.' MA Dissertation (Unpublished), University of Dar es Salaam.

Kahigi K.K. (1994). Lugha Katika Vitabu Vya Watoto. Katika *Kioo cha lugha: Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu, Na. 1. (uk. 21-36).

Kombo, D.K. and Tromp, D. L.A, (2006). *Proposal and Thesis Writing: Intoduction*, Kenya, Paulines Publications Africa.

Kothari, C. K (1990) *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C.R. (1993). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kvale, S.(1996). *Interviews An Introduction to Qualitative Research Interviewing*. London: Sage Publications.

Lakoff, G. and Johnson, M. (1988). *Metaphor We Live By*. Chicago: University of Chicago Press.

Lee, R.M. (1993). *Doing Research on Sensitive Topics*. Londo:Sage.

Ligembe, N.E.G (1995). *The uses of metaphor in Penina Muhando's Lina ubani.A stylistic analysis.* MA Dissertation,(Unpublished) University of Dar es Salaam.

Lofland, J., &Lofland, L. (1995). *Analyzing social settings: Aguide to qualitative observation and analysis* (3rd ed.). Boston: Wadsworth.

Malangwa, P.S (2010). "Handling Technical Translations: The Case of Translatins of Computer Programs from English into Kiswahili." Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa),Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Momanyi, C. (1991). "Matumizi ya Taswira kama kielelezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al-Inkishafi". M.A. Thesis. Nairobi. Kenyatta University.

Momanyi, C. (1998). "Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili". Ph.D. Thesis. Nairobi. Kenyatta University (Unpublished).

Momanyi, C. (2001). Nadharia ya Uchanganuzi Nafsia katika Mtazamo wa Kike na Uhakiki wa Kifasihi: *Kioo cha lugha.* Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Momanyi, C. (2007). "Patriarchal Symbolic Order: The Syllables of Power as Accentuated in Waswahili Poetry." *The Journal of Pan African Studies*, Vol.1, no. 8.

Mponguliana J. A. J. (1982). "The Development of Film in Tanzania" (Unpublished, MA Theatre Arts Dissertation) University of Dar es Salaam.

Mulokozi, M. and Kahigi, K.K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mutembei, A. (2009). UKIMWI katika fasihi ya Kiswahili 1982-2006. Dar es Salaam: TUKI.

Njewele, D. C. (2007). "Manifestation of Cultural Performances in Traditional African Films" (Unpublished MA Theatre Arts, Dissertation) University of Dar es Salaam.

Notcutt, L. A. & Lathan, G. C (1937). *The African and The Cinema*: *An Account of the Work of Bantu Educational Cinema Experment*. London : Edinburgh House.

Padget, D. (2002). *Qualitative Methods in Social Work Research: Challenges and Rewards.* London: Sage Publications Inc.

Polit, D. F., Beck, C. T. and Hungler, B. P. (2001). *Essentials of Nursing Research: Methods, Appraisal and Utilization*, 5th edn. Lippincott, Philadelphia.

Powell, R. R. & Lynn Silipigni Connaway. (2004). *Basic Research Methods for Librarian* (Toleo la 5.). London: Sage Publications Inc.

Patton, M. 2002. *Qualitative Research and Evaluation Method* (Toleo la 3). London: Sage Publications.

Payne, T. E and Weber. D. I. (2007). *Perspectives on grammar writing*. Amsterdam/Philadelphia: John Benjamins.

Ramadhani, D. (2005). *The Uses of Metaphors in Mbogo's Ngoma ya Ng'wanamalundi and*

Hussein's Mashetani. A Stylistic Comparison. MA Dissertation, (Unpublished) University of Dar es Salaam.

Senkoro, F.E.M.K (1982). *Fasihi:* Dar es Salaam. DUP.

Schutt, R. K. (2006) *Investigating the social world: The process and practice of research*. London: Sage Publications.

Shule,V. (2004). "Effective Video Film Reducing Young Mens Gender Violence and Other

.H.I.V Risk Behaviours", (Unpublished M.A Theatre Arts Dissertation) University of DSM.

Silva, M. (1995). *Ethical Guidelines in the Conduct, Dissemination, and Implementation of Nursing Research.* Washington DC: American Nurses Publishing.

Silverman, D. (2005). *Doing Qualitative Research: A Practical Handbook* (Toleo la 2.). London: Sage Publication Inc.

Speziale, H.J. S. & Carpenter, D.R. (2007. *Qualitative Research in Nursing:*Advancing the humanistic imperative (4th ed.). Philadelphia: Lippincott.

Ukadike, N.F. (1994). *Black African Cinema*. Bercley: University of Calfonia Press

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Focus Publication Ltd. Nairobi Kenya.

Weiss, R. S. (1994). *Learning from strangers: The art and method of qualitative interviewing.* New York: Free Press.

^ [a b c d] Songa wa Songa (9 April 2012). "Fresh revelations in Kanumba death probe". *The Citizen Daily*. Retrieved 10 April 2012.

^ [a b c] "Kanumba funeral: Thousands mourn Tanzanian actor". BBC. Retrieved 10 April 2012.

^ "Biography". Retrieved 10 April 2012.

^ [a b] "Lulu charged with Kanumba's murder". *The Citizen*. 11 April 2012. Retrieved 12 April 2012.

^ [a b c] Saur et al, Mahir (2010). *Viewing African Cinema in the Twenty-First Century: Art Films and the Nollywood Video Revolution p.86*. Ohio University Press.

^ "Steven Kanumba on Oxfam's GROW campaign in Tanzania". *Oxfam East Africa*. 5 June 2011. Retrieved 10 April 2012.

^ "Farewell Kanumba The Great: Photos from the escort and final mass at Leaders Club". Bongo 5. Retrieved 10 April 2012.

^ Kanumba laid to rest, Mohammed Ugasa, 11th April 2012

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO I: Dodoso Kwa Ajili ya Walimu na Wanafunzi wa Fasihi
Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu Usawiri wa Ujinsia Katika Filamu: Uchunguzi wa Matumzi ya Lugha Katika Filamu za Kanumba. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa kijinsia katika lugha ya filamu za Steven Kanumba ili kuona ni jinsi gani lugha inatumika kusawiri masuala ya kijinsia na nafasi ya mwanamke katika jamii. Nitashukuru sana wewe kama mwanafasihi ya Kiswahili utaweza kujibu maswali ya dodoso hili kwa makini, uwazi na ushirikiano wa hali ya juu. Nitafurahi ikiwa utaijaza hojaji hii kwa tarehe tulizokubaliana. Tumia bahasha niliyokupa kuifunga hojaji yako kwani taarifa utakazotoa ni siri na zitatumiwa na mtafiti kwa ajili ya utafiti tu na si vinginevyo. Aidha, nakuomba usiwe na hofu yoyote katika ujazaji wa hojaji hii maana majibu utakayotoa yatatunzwa kwa siri. Usiandike jina lako mahali popote.

Sehemu ya Kwanza

Taarifa Binafsi za Mtafitiwa

1. Umri………………………………………………
2. Jinsi………………………………………………
3. Kazi (Kitengo)…………………
4. Kiwango cha elimu…………………………
5. Uraia…………………………………………
6. Mahali unakoishi……………………………

7. Lugha yako ya kwanza ni…………………………

Sehemu ya Pili

Taarifa Kuhusu Matumizi ya Tamathali za Semi katika Mashairi ya Shaaban Robert

8. Taja vipengele vya lugha vilivyotumika katika filamu ya Johari, Moses na my Valentine.

   i) ....

   ii) ....

   iii) ....

   iv) ....

   v) ....

   vi) ....

   vii)...

9. Taja nafasi ya mwanamke kama inavyobainishwa na vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba

   i) ....

   ii) ....

   iii) ....

   iv) ....

   v) ....

   vi) ....

   vii)..

10. Je, vipengele vya lugha vilivyotumika vinabainisha tofauti za kimahusiano baina ya mwanamke na mwanamme.

i) ....

ii) ....

iii) ....

iv)..

v)...

vi)..

vii)..

ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO

KIAMBATISHO II: Mwongozo wa Usaili Kwa Ajili ya Wigizaji na Waongozaji wa Filamu

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Usawiri wa Ujinsia Katika Filamu: Uchunguzi wa Matumzi ya Lugha Katika Filamu za Steven Kanumba**. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa kijinsia katika lugha ya filamu za Steven Kanumba ili kuona ni jinsi gani lugha inatumika kusawiri masuala ya kijinsia na nafasi ya mwanamke katika jamii. Nitashukuru sana wewe kama mwanafasihi ya Kiswahili utaweza kujibu maswali ya dodoso hili kwa makini, uwazi na ushirikiano wa hali ya juu. Nitafurahi ikiwa utaijaza hojaji hii kwa tarehe tulizokubaliana. Tumia bahasha niliyokupa kuifunga hojaji yako kwani taarifa utakazotoa ni siri na zitatumiwa na mtafiti kwa ajili ya utafiti tu na si vinginevyo. Aidha, nakuomba usiwe na hofu yoyote katika ujazaji wa hojaji hii maana majibu utakayotoa yatatunzwa kwa siri. Usiandike jina lako mahali popote.

1. a) Una umri gani?

   b) Kiwango chako cha elimu

   d) Ulianza kuitumia kuigiza/kuzalisha filamu lini?

2. Miongoni mwa mambo yanayoweza kutambulisha mahusiano ya kijinsia katika kazi mbalimbali za kifasihi ni pamoja na lugha. Ni aina vipengele vipi vya lugha vilivyotumika katika filamu za Kanumba

   i. ....

   ii. ....

iii. ....

3. Je vipengele vya lugha vilivyotumika katika filamu za Kanumba vinasawiri masuala ya kijinsia?

4. Je ni mahusiano ya aina gani yanayojitokeza katika tamathali za semi zilizotumika katika filamu za Kanumba

5. Je, Mwanamke anapewa nafasi gani katika filamu za Kanumba

6. Je unaweza kusema Kanumba ana mtazamo hasi juu ya mwanamke?

ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO

KIAMBATISHO III: **Maswali ya Mwongozo wa Majadiliano ya Vikundi**

1. Unafikiri ni kwa nini Kanumba ametumia vipengele vya lugha katika filamu zake?

2. Je, unadhani vipengele vya lugha vilivyotumika vinasawiri suala la ujinsia katika jamii?

3. Jadili tofauti za kijinsia baina ya mwanamke na mwanaume kama ambavyo vinasawiriwa katika mashairi ya Kanumba.

4. Je, vipengele vya lugha vinasawiri nafasi ya mwanamke katika jamii?

5. Jadili nafasi ya mwanamke kama ambavyo inasawiriwa na vipengele vya lugha katika filamu za Kanumba

6. Taja vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika filamu za Kanumba

7. Je lugha anayoitumia kumuongelea mwanamke inatofautiana na lugha anayoitumia kumuongelea mwanaume

ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO